*Katika Kanisa ambalo Yesu anaonekana kwamba yuko sasa, anahusika, na yuko Hai, badala ya masalio ya kihistoria kupendwa na kuheshimiwa na kufunzwa kuihusu, kuna Uhuru.*

*Kila mtu ambaye Yesu anaishi ndani yake na anayetumika hivyo kila siku kati ya Waumini, ana jukumu la kutoa Vipawa vyao "ili kuadilisha Mwili." VYOTE vya Yesu vilimiminwa juu ya Mwili Wake, kwa Vipawa Vyake VYOTE—na Kipawa chochote kinaweza kuhitajika wakati wowote.*



# YESU


UKWELI—SI MABAKISHI,

UKWELI—SI BIDHAA ZILIZOTENGENEZWA

KICHWA—SI KIUMBE MKUU

© 2007 Haki Zote Zimehifadhiwa. Vitabu vyote na sauti zinapatikana bila malipo, kama zawadi kwa Yesu na wale ambao watatoa maisha yao kwa ajiili Yake. Wasiliana nasi kwa anwani ya barua . Na Neema Yake na Uzima Wake uwe juu yako, unapovaa Jina Lake na Kutembea katika Njia Zake.





# Mwaliko Wake

Mualiko wa Mungu kwa dunia ni kuwa nyumbani pamoja kwa ajili ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu— kuwa Bi harusi aliye jitayarisha kwa kurudi kwa Bwana harusi,Yesu Kristo (Yohana 13-15, Waefeso 2-5, Ufunuo19:7) Ukitafakari kuhusu picha zilizo kwa maandishi ya vile maisha yalivyo, naye au kumhusu, Yesu anatamatisha —je ni nini? *Ni uchumba—na chakula cha harusi!* Mungu anatuhimiza akisema "Nina uhakika Kunihusu. Ikiwa mtakuwa ndani Yangu na kuangalia niliye hakutakuwa na washindani wengine wowote duniani. HAkuna kitu chochote duniani ambacho kita shinda roho yako kama vile ninaweza—kwasababu nilikuumba kwa ajili yangu Mimi Mwenyewe. Vitu vingine vimekupotosha lakini ikiwa utachukua mda na kukanyaga kando Nami, utaona jinsi maisha yanavyo takikana kuwa. Na kutakuwa na harusi!

*"Kwa hivyo jitayarishe,bi harusi"*

Kutoka wakati wa mwanzo, ualiko huu umeleta watu kumtafuta Yeye.Ualiko huo Wake ni kwetu pia.Na hayo ndivyo yalivyo. Hii si funzo la nje.Ni mchoro na kuhadaa yale yaliyo ndani yetu. Ni sisi kutazama kwa yale yote ambayo ni Yeye Anayoyasema.

Siwezi kuishi bila Yeye au na yale yaliyo mazuri na muhumu Kwake. Sitaki kuishi bila hayo! Singependa kuota kuishi nje ya Mapenzi yake kwa maisha yangu au nje ya sababu Zake. Nataka kumfuata Mwana kondoo popote aendapo. Chochote Anachotaka kwa maisha yangu, Anacho! Ni mkate wa uzima,ambapo uhakika wangu wote na umefanywa kupatikana. Ni picha ile ambayo ni ya uongozi na ukarimu na wakusamehea na wa huruma ambayo siwezi kuishi bila—*ambayo sitaki kusishi bila.* Nataka kumuona Akiwa na nguvu. Nataka kumuabudu. Nataka kumuona na upendo. Nataka kumuona mwenye hekima kupita kiwango cha maneno. NA, NATAKA KUWA NAYE! Nataka kusikia kila neno analotaka kulisema. Sitaki kabisa kuwa hatua moja kutoka Kwake kwa maisha yangu yote. Siwezi kumgeuzia mgongo kwasababu ya uchoyo, maringo au uvivu au za hisia za kuumiza. Siwezi kumugeuzia mgongo. Majaribu yapo lakini kupoteza ni kuu sana.

Yesu anazo hizo sifa zote.Ako kwa njia1,000 tofauti na hekima kupita maneno. Huyu ni Mwongozi.Huyu ni Yesu. Hii sio hadithi. Hii sio hadithi huko nje juu ya miungu ambao waliumba dunia na kuketi juu ya kiti kikubwa cheupe cha enzi. Hii ni juu ya Utu wa Yesu na Baba Yake ambaye anatuongoza sisi wote. Tukiangalia,tukipata wasia wa kukutana naye, hakuna njia ya Kumzuia kabisa. Shida imekuwa ni ukosefu wa kujitolea na kutuwacha sisi wenyewe ndani ya uwozo na Mikono Yake ya ukweli.Ukweli wake ni zaidi ya uaminifu. Lakini kila wakati hatuendi karibu kuona, kwa sababu tunajiweka sisi wenyewe kuwa na kazi nyingi, wachoyo, kutojali sana—na hatutaki kuchukua wakati kuangaziwa au kuvutiwa naye.

Baba anajua kuwa tukichukuwa wakati kuwa naye ndani ya Mwanawe,Basi ataonyesha tabia yake kwetu kwa njia hii ambayo haitazuilika. Sifa za tabia Yake zinasitasita.Kuna kitu juu a kuwa Naye kitakacho kututua dhidi ya vitu vingine ambavyo vitakuwa



mzigo na kukuvuta chini.Punde,unashangazwa na kitu ambacho kiko nje ya eneo la kuenea kwa ustadi wako. Naye ni YESU! Na, anatukaribisha kuja kutembea naye. Atakuangazia na sifa zake za utukufu,huruma na kusamehewa daima dawamu.

Utaona Akitabasamu na mwangaza katika macho Yake.Utaona vile upepo unavuma kupitia kwa nywele yake.Utaona, kusikia, na kushuhudia vitu ambavyo vitakupeleka hadi kwa eneo lingine, na wakati hautakuwa hapo tena(Ufunuo 1:12-18).Utaona uongozi Wake na nguvu Zake. Utaona vile Atakavyoamua dhidi ya dhambi. Utaona vile Ana mwelekeo na maono angavu ya vile maisha yanavyo stahiki kuwa. Na utasikia undani wa kicheko Chake na uhisi ujoto wa motisha na kukumbatiwa.

Njoo umfuate. Atakuonyesha uongozi. Atakuonyesha nguvu. Atakuonyesha tabia zisizo tingizika na hulka jinsi maisha yatakavyokung’arisha na kukufanya wewe kuja naye kwa sababu hautakuwa hatarini .Na uko mahala pema Alipo.Atakuonyesha ukarimu wake na unyenyekevu ambayo itakuelekeza katika roho na maisha. Ukija Kwake na utubu dhambi zako atakuosha na kukutakasa na kuweka roho Yake ndani yako.Sasa, atatoa almasi na yakuti na madini yaliyoko. Atatoa vitu hivyo,Atakufanya uwe malkia, Atakufanya uwe mfalme.

Anataka kujenga jeshi la wafuasi lakini sio la wale wasio hitimu ekevu kutumiwa_kisheria—“Nifuateni au mtaenda jehanamu”. Hiyo ni kweli lakini halihusiki na yale Yesu alikuja kuonyesha wafuasi wake kumi na wawili. Je, unafikiri walimfuata Yesu kule kote mashambani alikoenda kwa sababu alikuwa anaonyesha kidole kwao na kuwaambia wamfuate au wataenda jehanamu? Je, unakumbuka maandishi kama hayo? Je ni hivyo ndivyo Alivyofanya alipoenda na kumwomba Baba usiku wote? Je, alisema Baba nionyeshe nitakalo sema na akasimama na akasema “nyinyi wafuasi wangu kumi na wawili njooni nami au mtaenda jehanamu?” Hapana.*Walitaka* kuwa Naye kwa sababu waliona kitu kumhusu ambacho kuliwashangaza, waliona hekima Zake na uvumilivu. Waliona uongozi dhabiti na tabia zisizobadilika. Waliona mtu ambaye atachukuwa upigo wa maisha na kusimama

wima pamoja na kicheko kidogo kwa uso wake, na ujasiri kwa macho Yake. *Na walitaka kuwa kama yeye -. Walitaka kuwa naye!* Hawakuwa wanaenda mahala popote kwa sababu hapakuwa na mahali popote walitaka kwenda ila kuwa kando Yake (Mathayo 4:19-22,Yohana 5:68 Matendo 5:20, Matendo 3:19-20)

Hakutaka kuwaugofya na Hatuogopeshi sisi pia. Anatukaribisha kumwona Yeye kama vile alivyo na kuona maajabu ya matendo na maajabu ya ubihafsi yale aliyonayo….ili ndiyo tuwe Naye, kwa maisha haya na yajayo.Ningependa niwe kama Yeye nikiwa mkubwa.

Kabla mda mrefu Yesu atakuja kumchukuwa bi harusi ambaye yuko tayari. Naye, kwa kutaka kwake Baba kwetu si *kuhudhuria* bi harusi bali ni kuwa bi harusi….si *kuhudhuria* nyumba bali ni *kuwa* nyumba.Ukirejelea Agano La Kale, utaona haja Yake imekuwa na nyumba; bali si ya waliokolewa kwa kutaka kwake ila kupenda kwake kwa mahala ambapo Angeishi hapa duniani Aliyoumba. Yesu anatuambia katika kitabu cha Luka 17 ya kuwa ulimwengu Wake hauko hapa au pale, lakini uko ndani ya *watu waliopanua mahala pa nyoyo zao,* kuondoa mambo ya ulimwengu, hisia za kimwili hamu na ndoto ni lazima tuwe wale walitegeneza nafasi ya Yesu katika nyoyo zetu kama vile Yesu alivyotufunza katika kitabu cha Yohana 8. Na hiyo ni maumbile ya Ekklesia mwili wake unavyoishi na kanisa.

Yesu hakuja kusamehe dhambi kwa uzuri kama huo au kutufanya tufikirie juu ya mafunzo Yake. Yesu alikuja ili tujuwe maisha yaliyvo sawa na Baba ambayo alishudia—sio tu kuishi hapa, kufa, na tena kupaa mbinguni. Kama vile Bibilia inavyosema, alikuja hapa ndivyo tuishi "kwa nguvu ya maisha Yake yasiyo haribika" kushudia usawa wa ushirika na maisha na upendo pamoja na baba na nduguze vile Yesu alivyofanya.

"Kuokoka" ni MBALI sana na mwisho wa hadithi.Kulingana na kuzaliwa kwa Yesu, kuzaliwa kwetu Ni Kianzo tu cha hadithi ambayo Baba anataka kusema ndani yetu (Wakolosai 1:26-29, Wagalatia 4:19, Yohana 7:37).Nia au mapenzi Yake ni kwamba Yesu ametengenezwa ndani yetu na kwamba sisi (watu wote, Bi



Harusi, Nyumba Yake) zitakuwa dhibitisho ya Utukufu wa Yesu wa Nazerethi hapa duniani wa kisasa**.** Katika ziku hizo. Nia ya Mungu siyo kwamba Yesu aonekane ndani yao, lakini ati kwa PAMOJA, muungano na tutaweza kuwa waakilishi wa Yesu.

Na, kufanyika kwa hayo yote "kutafuta utajiri" uko na kila kitu kuhusu vile tunaishi maisha yetu ya kilasiku pamoja. Mengi ya dini na Ukristo zimefanywa kwa miaka mingi ni kutufunza maandiko *kumhusu* Yesu na Kanisa.Ni wakati wa kuendelea kujifunza mafunzo *ya* Kanisa na *uumbile* wa kanisa.(Waefeso 3:10, Mathayo16:18)

Tunaweza TU kuwa kanisa Lake na kuishi maisha Yake tunapopendana na kubadilisha maisha yetu na wengine kila siku. Tunasaidiana kumjua Yesu vizuri kwa kusaidiana, kuepukana na dhambi, kupendana na wengine, na kujali maslahi ya wengine. Vile tunavyo jijali. Haya ni mafundisho ya Yesu. Hivi ndivyo alivyoishi maisha yake kwa ajili ya sisi na ametuita tuishi hivyo kwa ajili ya wengine. Hivi *ndivyo* Bi harusi anavyo "tayarishwa" kwa kurudi kwa bwana Harusi Yesu. Kila mara tunakuwa warembo tunavyo jifunza jinsi ya *kupendana kwa ukweli.* Tunapoweka kando ile ubinfsi na maringo yetu inayotugawanyisha na wengine, na tunapo fungua mioyo yetu ionekane na wengine, Roho mwema**,** wema wa Mungu na upendo wa Mungu unamwagika juu yetu…. na tunafanywa Bi harusi aliye *tayari* kwa kurejea kwa Bwana Yarusi Yesu Kristo.

Hili ni Kanisa—kuishi hivi kila siku, *kutohudhuria* nyumba ya Mungu, lakini *kuwa* mahali Mungu anaishi. Kwa hivyo nyumbani kwetu, mahali petu pa kazi, na Kanisa letu lote zipo pamoja. Hakuna tena vizuizi ndani ya roho yangu kwako na hakuna vizuizi katika ya nyumba yangu na yako. Naweka kando ubinafsi, maringo,uvivu na kutoamini na ninawapenda wengine jinsi Yesu alivyo nipenda mimi. kila mtu anapofanya hivyo, kutoka kwa mdogo hadi mkubwa yesu anatumwagia mafuta ya uponyaji na tunakuwa kanisa. Bi harusi mrembo. Yesu hakuja kutufanya sisi kuwa werevu. *Alikuja kutupa maisha kikamilifu—Kuishi maisha yake kilasiku kati yetu, sio kutamka maneno yaliyo*

*ombwa, kuimba nyimbo na kuomba maombi yalivyo ombwa, kuimba nyimbo na kuomba maombi yalivyochafuliwa k.m. kioo kilichochafuliwa.MAISHA!*



# YESU:
# *Mjenzi na Mbuni*

## Kujenga Na Nyenzo Nzuri

### *Je! Kanisa Na Mkristo Ni Nini?*

Biblia inafunza kwamba Mungu haishi katika nyumba zilizojengwa na mikono ya mwanadamu. Waefeso 2 pili na vifungu vingine vingi vya Biblia vinasema kwamba *sisi* ni nyumba au makao ya Mungu kwa Roho—Kanisa. Unapotembea au kuendesha gari barabarani, unaweza kutambua jengo la kidini kwa sababu linaonekana kama jengo la kidini. Bali, kwa kuwa Kanisa la kweli ni watu, ***na wala sio jengo,*** basi kwa ***kweli*** linafanana aje? Unawezaje kutambua t0fauti kati ya Kanisa la kweli na la uongo?

Katika "kanisa" la Agano la Kale, unakuwa mshirika kwa sababu ya vile wazazi wako walivyokuwa (Wayahudi). Ikiwa kwa kawaida uliamini jambo adilifu na wazazi wako walikuwa sehemu ya kanisa hili, na wewe "ulihudhuria kanisa" mara kwa mara na kutoa fungu la kumi, hivyo basi ulikuwa mshirika wa "kanisa." *Katika Kanisa la Yesu la Agano Jipya, hii si kweli—* ***lazima utoe roho yako kwa Mungu.*** Unabii kuhusu Agano Jipya ulisema kwamba kanisa ambalo Mungu hujenga (Yer. 31, Waeb. 8, Waeb. 10) ndilo Kanisa la kweli, na *kuanzia mdogo hadi mkubwa, washirika wake WOTE watamjua Mungu Aliyehai.* Kanisa linaweza kufahamika kwa njia hii TU. Chochote chini yake kinaweza kumaanisha vyema na kufanya mema na ya kidini (ikihusisha watu wengine ambao Wameokoka), lakini SI kanisa la Yesu Kristo, jengo la mtaani, ikiwa tu ni watu "wanaohudhuria" kitu kilichopangwa kwa kalenda bila kuunganisha kila siku Maisha ya pamoja (1 Wak. 12).

Kanisa la kweli lililojengwa na mawe yaliyo hai ambalo Yesu anaangalia na kulipenda lazima lijengwe na nyenzo nzuri. Ikiwa jengo lolote limejengwa na nyenzo mbaya, unajua kwamba litaanguka. Ikiwa mbao ambayo imeshikilia paa imeoza, itaanguka. Matofali ambayo ni mepesi, yaliyoundwa vibaya, au yaliyoundwa na nyenzo mbaya hayawezi kumudu uzito na yataanguka. Vivyo hivyo, tukijaribu kujenga nyumba ya Mungu na nyenzo mbaya, hiyo pia itaanguka. Ikiwa mtu kwa kweli *hamjui* Mungu, hawezi kuwa mshirika wa Kanisa la Yesu. Ikiwa nyumba ambayo Mungu anajenga kutoka kwa wanaume na wanawake itaweza kusimama, ni lazima isiwe na mawe mbaya ndani yake (1 Wako. 3-5).

Kwa hivyo, je! Ni lazima Kanisa, au watu wake wawe wakamilifu? Kwa kweli hiyo haiwezekani (1Yohana 1). Lakini kulingana na Neno la Mungu, kinachohitajika ni hiki: Asilimia mia ya washirika..“wanapenda Nuru” na “wanapenda Kweli” na kwa hakika wamemuona Mungu Mwenyewe kwa njia ambayo “mnofu1 na damu haijafunua.” NDIO, ***hii inahitajika (Mat. 16:16-18, Yohana 3:19-21, 1Yohana 1-3, Eze. 11:19, Eze. 36:26, Yer. 31:34).*** Hayo ndio Yesu alisema atajenga Kanisa LAKE juu yake, ikiwa litakuwa Kanisa LAKE. Kitu kingine chochote kitakuwa kama kujenga nyumba na tofali nyepesi au mbao iliyooza. Nyumba ambayo Yesu anatengeneza ndiyo nyumba nzuri kabisa ulimwenguni, na Yesu atatumia nyenzo za kweli na nzuri tu ili kujenga Nyumba Yake.

Mara nyingine, hii HAIMAANISHI kwamba kila mtu ni mkamilifu. Bali, inamaanisha kwamba kila mtu anataka kumpenda na kumtii Yesu na hapuuzi usaidizi kutoka kwa wengine ambao wanataka kumsaidia kumpenda na kumtii Yesu; wanataka usaidizi huo. Nyenzo nzuri za ujenzi wa Nyumba ya Mungu ni wakati mtu “anapenda nuru”, kulingana na Yesu Mwenyewe. Nyenzo mbaya za ujenzi, kama vile mbao iliyooza, ni mtu ambaye hataki usaidizi huo. Mtu huyo husema, “Usinihukumu. Shughulika na mambo yako.” Hao husema kwa kujitetea, “Toa gogo lilioko kwa macho yako mwenyewe.” Hiyo ni nyenzo mbaya ya ujenzi, ambayo Mungu alisema haikubaliki katika Nyumba Yake. Yesu hatajenga nyumba Yake kwa njia



hiyo. Hiyo ni mbao iliyooza na itakatwa kabisa kutoka kwa watu (Matendo ya mitume 3:23, Mat. 18, 1Wak. 5). Katika kanisa la Kweli, mtu anayefanya hivyo hajakaribishwa. Haijalishi pesa wanazo au vile wanavyofahamu Biblia zao vyema. Wanaweza hata kuwa “viongozi,” lakini ikiwa hawataitika kwa wepesi kwa mafunzo ya Yesu, hivyo basi hawawezi kuwa sehemu ya Kanisa la kweli la Yesu ambalo linajengwa Kiroho. wakikataa upendo na maombi, hekima, usaidizi na uvumilivu, basi kuwaruhusu waendelee kuwa kati ya watu wa Mungu itakuwa kumpinga Yesu na pia kupuuza amri Zake.

Ikiwa mtu ameokoka, ATAKUWA na Roho Mtakatifu (War. 8:9, Wag.3, Waef. 1). Na DHIBITISHO kwamba ana Roho Mtakatifu ndani yake (haijalishi ni mara ngapi amekuambia “ushuhuda” mkubwa na kusema, “Bwana, Bwana!” Mathayo 7) ni kuwa anapenda kutii. Hao ni viumbe vipya na sasa wanapenda Nuru, na wanapenda Kweli (2Wathe. 2:10), na “kama watoto waliozaliwa ” “wanatamani” Neno la Mungu ***litumike katika maisha yao (1Petro 2).*** Ikiwa mtu ana Roho Mtakatifu, atapenda Nuru na atapenda Kweli…. na kisha tabia yake itaanza kubadilika. Atatubu kwa jinsi anavyomshughulikia mume wake au mke wake, na atabadilika. Atatubu kwa jinsi anavyowashughulikia wafanyakazi wenzake, au watoto wake, au majirani wake, na atabadilika. Atatubu dhambi zake za zamani na tabia zake mbovu, na atabadilika na atakuwa amekomaa zaidi.

Kipawa cha Roho Mtakatifu ni stakabadhi ambayo inadhibitisha urithi wake. “Huu ndio uamuzi,” asema Yesu, katika Yohana 3. Hii ndiyo inatofautisha kutokuwa na hatia na kuwa na hatia. Si kwamba kila mtu ni mkamilifu, lakini wale WOTE ambao dhambi zao zimesamehewa “wanapenda Nuru.” Wanakipawa cha Roho ambacho hawakuwa nacho zamani. Sasa, kutoka ndani, mioyo yao ya jiwe imefanyika mioyo laini ya nyama. Kutoka ndani, Mungu anawasababisha kuweka amri Zake na makataa. Kutoka ndani, wanajali kuhusu maneno ya Yesu kuhusu tabia zao. Kondoo hujua sauti ya Mchungaji kwa sababu wana Roho ya Yesu. Kondoo husema, “Ninataka kumfuata Yesu! Niongoze njia hiyo.” Mbuzi husema, “Achana na mimi! Ninaweza kufanya

miujiza! Ninaweza kupeana pesa zangu kwa masikini! Ninajua mambo. Mimi ni mzuri kukuliko, na sijali unachosema."

Mkristo, mshiriki wa Agano Jipya, anapenda Kweli (2 Wathes. 2:10) na anapenda Nuru (Yoh. 3:19-21), na sasa ni "mshiriki wa asili KUU " (Petr. wa pili mlango wa 1:4, War. 6:1-14). Hilo ndilo dhibitisho kwamba Roho anaishi ndani yao au kati ya mmoja wetu yeyote. Si lazima tuchukue neno la kila mtu kwa sababu anasema, "Bwana! Bwana!" ***Ni mtu yule aliyewacha nafsi yake na maisha yake kwa ajili ya Yesu TU, na Ameguwa na Mbingu na Muumbaji wa Ulimwengu anaishi ndani yake ndiye kwa kweli ameokoka, na ni "mshirika" wa Kanisa Lake la mtaani*** (War. 8:9-11, Lk. 9:57-62, Yoh. 1:12-13, 3:16-21,1 Yoh. 3:8-10, 5:18-20).

Jengo la Kweli, Kanisa halisi, LIMEDHIBITIWA NA wale ambao wamekuwa na ufunuo wa Mwana "ambao nyama na damu haikufunua (yaani asilimia 100 ya "washirika"!), bali Baba Mwenyewe aliye Mbinguni aliwafunulia." Si kuhusu kukaribiana au ufahamu au "kujitolea" au malezi. Ni kuhusu kukabiliana kibinafsi na Mungu Baba, katika Utu wa Mwanawe, ambapo mauti hutoa aina ya Uzima wa Mungu, Maisha ya *Zoe*, kutoka kwa kitu kisichopo (Yoh. 3:5-8, Yoh. 12:24, War. 6:1-14, Wag. 6:14-17). Kwa kweli kuna wachache wanaohitaji "ustarabu maalum" na wengine ambao wanaamua katika "mwaka wao mmoja zaidi" (Yohana 13:8-9, Yohana 15, 1Yohana 2:19, Yuda 11-25).

Aidha, tuna maisha YASIYO ya kawaida na Yeye na sisi kwa sisi, au SI Ukristo wa Kibiblia na SI Kanisa halali. Kwa hakika kuna watu wengine ambao Wameokoka "wanaohudhuria" mashirika ambayo kwa kweli si makanisa, ijapokuwa wanajiita makanisa. Hilo ni suala tofauti. Kwa urahisi tunasema kwamba hatutagusa Kiti Chake cha Enzi (tutaguza tu hisia zisizo dhahiri za *"akili"* yetu) ikiwa hatutaishi Pamoja kila siku—*Maisha ya ZOE*—muda baada ya muda tukiunganishwa kwa Kichwa na yule mwingine! Karamu ya "huduma" ambayo "inafanywa kwa heshima Yake," au kujifunza kweli kumhusu yeye, au kuita hisia kutoka Mbinguni na muziki wetu—kihistoria, hizi zimebadilisha maisha machache



sana kuwa Mfano wa Mwana. Aidha tunashiriki katika Nguvu za Kichwa cha Mungu kwa pamoja kila siku, au sio Maisha ya Milele, au Jengo na Kanisa, kama vile Mungu atakavyo. "Chachu ndogo huchachua mkate MZIMA."

Lazima tusiwe watoto tu ambao husema mambo yanayofaa, na hatuishi kama Yesu. Na, Kanisa sio mkusanyiko wa Wakristo wa uongo ambao wanasema mambo yanayofaa lakini hawana Roho wa Yesu anayeishi ndani yao, kama Mtu. Yesu ni Mjenzi mkubwa. Hatajenga na mawe mepesi au mbao iliyooza. Anataka kujenga Nyumba ya kuishi yenye Utukufu—moja ambayo inamfaa Mfalme kama Alivyo. Kwa hivyo nyenzo za ujenzi katika Nyumba ya Mungu lazima ziwe nzuri kabisa. Kanisa la kweli lililojengwa na Mungu, wala sio mikono ya mwanadamu, limejengwa na mawe yaliyohai—Wakristo wa kweli—kinyume na mawe yaliyokufa, matofali au nyasi. Yesu atajenga tu na nyezo nzuri za ujenzi . Ikiwa ametuoa katika Agano na Kiapo, tukawaacha wapenzi wale wengine wote, tukazaliwa mara ya pili, tuna mioyo nyepesi, tunapenda mafunzo Yake, kwa kweli tunataka kubadilisha mambo katika maisha yetu ambayo yanahitaji kubadilika, na tuelekeze nyuso zetu Kwake wakati wa shida au ugumu, tukimuuliza Yeye na ndugu na dada zetu kutusaidia sisi, basi sisi ni mawe maridadi yaliyohai ya Nyumba ambayo Yesu anaishi. Tunaweza na tutakuwa Bi-arusi wa Yesu wenye utukufu. Hii ndiyo Habari Njema ya Ufalme wa Mungu.

## Kujenga Kwa Mtindo Wake Na Mbuni Yake

### *Maisha Ya Pamoja Ya Kila Siku*

Sasa kwa kuwa tumefafanua nyenzo nzuri za ujezi wa Nyumba ya Mungu ni nini …zingatia hii: Kisia tuchukue mawe yote mazuri, mbao zote nzuri, na nyenzo zote nzuri, zinazofaa za ujenzi ambazo Yesu amechagua kwa ajili ya Nyumba Yake na tuweke nyenzo hizo zote nzuri kwa fungu. Kisia nini? Bado hatuna nyumba. Nyumba ya Mungu inahitaji zaidi ya nyenzo nzuri za ujenzi (Wakristo wa kweli). Kwa sababu una nyenzo zote za nyumba zilizorundikwa katika fungu haimaanishi kwamba una nyumba ya kulala. Fungu

hilo halitakulinda kutokana na dhoruba, haijalishi vile nyenzo hizo zinaweza kuwa nzuri.

*Ndiposa iwe Nyumba nzuri ya Yesu kuishi, Nyumba ya Mungu lazima ijengwe pamoja kwa kutumia* ***Mtindo*** *Wake na* ***Mbuni*** *Yake. Nyumba Yake ina watu, Mawe yake yaliyohai, na* ***ana njia ya pamoja ambayo lazima tujenge maisha yetu.*** *Maandiko humwita Yesu Mjenzi Mkuu. Tunastahili kujali sana kuhusu Ramani Yake, Mpango Wake.*

Mungu ana watu wengi wazuri ulimwenguni kote. Kile ambacho kimetendeka mara kwa mara katika miaka 2,000 iliyopita ni kwamba watu hawa wamekuwa wakitamani kubadilisha maisha yao na kumpendeza Yeye, lakini wametatizwa. Wameshindwa kupata uwezo wao wote na kwa kweli kumtumikia vizuri. Ni moyo wao wote, lakini wanashindwa tena na tena. Sababu ya hao kushindwa ni kwa sababu mara kwa mara tunajenga kwa njia isiyofaa. Hatujajenga kulingana na mtindo, mbuni, ambayo Mungu ametupa. Wakati mtu yeyote anapojaribu kitu chochote, lakini anajaribu kukifanya kwa njia isiyofaa kabisa, ni nadra yeye hufaulu, haijalishi vile yeye ni mwaminifu.

Nyumba ya Yesu imejengwa kwa mtindo *Wake*, sio wetu. Na mtindo Wake ni "baba, mama, ndungu, na dada mia moja." Mtindo wake ni kuwa tuweze "kukiriana dhambi zetu" na tuponywe. Mtindo Wake ni kuwa tuweze "kuchukuliana mizingo na kwa hivyo kutimiza sheria ya Kristo." Mtindo Wake ni kuwa tuweze kuwa "kitu kimoja, kama vile Yeye na Baba ni kitu kimoja." Haja ya Mungu si mawe ya kando ambayo huja pamoja siku ya Jumapili ili "kuhudhuria" hotuba au karamu, lakini haja Yake ni familia ambayo imejengwa kwa pamoja kila siku, iliyounganishwa katika maeneo yote ya maisha ya kila siku, kama Familia.

Yesu amechagulia Nyumba Yake mtindo ambao unafanana katika kila nchi, haijalishi lugha au utamaduni. Mtindo huo ni kuwa watu wote wa Mungu watoe maisha yao kwa ajili ya kupendana na kuhudumiana kila siku, kama Familia, kwa pamoja. Kanisa la kweli la Yesu, liliunda njia Yake iwe yenye nguvu, lazima iwe



Familia kila siku. Wanakula pamoja kutoka nyumba hii hadi nyumba ile nyingine, wanatumikiana na kusaidiana kwa njia nyingi kila siku. Wanazungumza neno la Mungu wao kwa wao kila siku ili kuwasaidia kuwa zaidi kama Yesu. Wanapoona dhambi, wanaenda kutembea na kuzungumza kuihusu kwa pamoja. Hawasubiri "Jumapili" ili wasikilize mtu akihubiri mahubiri kuihusu. Kusudi la Mungu (Waef. 3:10, 1Petro 2) ni kuwa sisi wote ni makuhani wa kila siku na wajumbe wa Mungu kwa yule mwingine "tunapoinuka, kukaa chini, na kutembea njiani."

Sisi wote tumeitwa kuwa makuhani wa Yesu. Sisi wote tumeitwa ili kubeba neno la Mungu na kusaidiana. Hii inamaanisha kwamba ukimwona jirani yako akiwa mchoyo au mwenye hasira, au ukimwona akinywa, au mwenye kiburi ambacho kinavunja moyo wa Yesu, basi kila mmoja wetu atachukua jukumu la kusaidiana ili tubadilike. Hii ni ya kila siku. Haina lolote na kufanya na Jumapili. Kanisa la kweli la Yesu limeundwa na Mawe yaliyo hai, na mtindo wa Nyumba hiyo ni Familia ya kila siku. Si jambo ambalo "tunahudhuria," bali ni vile tulivyo kila siku.

Je! unaona vile hizi zote zinaunganika? PAMOJA NA MAHUSIANO YA KILA SIKU TU ndio unaweza kujua ikiwa kuna mtu anayependa Nuru na Kweli, na kwa hivyo ni mtoto wa Mungu. Mikutano chache kwa wiki haitamruhusu mtu yeyote kujua ikiwa mtu anapenda Nuru na ana udhaifu, au ikiwa anachukia Nuru na kwa hivyo hajaokoka. Mpango wa Mungu ni hazina katika vyombo vya kidunia. Mpango ya Mungu ni ukuhani wa waumini. Mpango wa Mungu ni ya watu Wake ili "waonyane kila siku." Kwa kweli tunapokuwa tukiishi hivi kwa pamoja, faida moja ni kuwa watoto wote wa kweli wa Mungu wanakomaa zaidi na zaidi. Matokeo mengine ya kutembea kwa pamoja kama vile Mungu alivyokusudia ni kwamba ikiwa mtu hapendi Nuru, hivyo basi anafichuliwa kama mnafiki. Ikiwa hawezi kurekebishwa, ikiwa hajali yale Yesu anasema kuhusu mambo haya, ikiwa anakasirika na ni mkatili, basi anafichuliwa kama Mkristo wa uongo. Inakuwa wazi kwamba lazima hakuwa kwa kweli ametoa maisha yake kwa Yesu kwa sababu ukweli ni kwamba mtu hawezi kuwa na Roho Mtakatifu na asipende Nuru (Yohana 3, 1Yohana 1, 3).

Tukijenga kwa njia hii—kwa kubadilisha maisha yetu ya uchoyo au ya uzembe, na kwa kweli kujifunza vile ya kupendana kama familia kila siku, kwa kuchukua jukumu la kutumikiana na kusaidiana na neno la Mungu—basi itakuwa Nyumba ambayo Yesu anaweza kuishi ndani na anaweza kuipenda. Itakuwa Nyumba yenye mbuni nzuri ambayo itakuwa rahisi kwa Yesu na kwa sisi wote kuishi na kufanya makao yetu.

Yesu alisema kwamba wakati tunapotumia neno Lake, wakati dhoruba inapokuja (na itakuja), basi nyumba hiyo itasimama. Itasimama kwa sababu imejengwa juu ya mwamba "kwa kutumia neno Lake," sio kwa kufikiria au kuimba kuhusu neno Lake. Tukiimba juu yake tu, kuomba juu yake na kuzungumza juu yake na tusibadilishe vile tunavyoishi ili tutii neno Lake pamoja na yule mwingine, basi wakati dhoruba inapokuja, haijalishi vile nyumba hiyo inavyoonekana maridadi, itaangushwa na kuangamia. Hii ndio Yesu aliahidi katika Mathayo 7. Kwa hivyo, hakikisha umejenga njia Yake na unafanya jambo kuhusu Kweli Yake. Zitii, na kisha dhoruba haitakuumiza.

Kwa njia ile ile ndege ndogo au sungura mdogo hujificha chini ya mwamba wakati dhoruba inapokuja, unaweza kujificha katika makao ya bawa la Yesu ikiwa utajenga vile anavyokuagiza. Dhoruba itatikisa miti na kusongeza vitu vizito. Itaziangusha na radi itapiga. Lakini kama utajenga kwa njia ya Yesu na umtazame Yeye wakati inapokuja, utakuwa salama katika makao ya mabaya Yake. Dhoruba nzito itapita na jua litang'aa. Ndege wataanza kuimba tena, na maisha yatakuwa safi na mapya. Itakuwa nyumba yenye nguvu sana na yenye Mbuni nzuri. Wakati dhoruba itakapokuja na kugonga Nyumba, itasimama *kwa sababu ina nyenzo nzuri tu, na kwa sababu mbuni ni nzuri.* Kutakuwa na uharibifu mdogo sana kwa Nyumba hii nzuri, na sisi wote tutakuwa salama. Kama vile Baba alikuwa dhahiri kuhusu nyezo na mbuni Nuhu alistahili kutumia ili kujenga Safina, hivyo pia Yesu ana mpango wa nyenzo na mbuni ya Nyumba Yake. Na Mpango Wake si, katika Makubaliano Mapya, mtu mtakatifu akitoa hotuba kwa shirika la watu "wanaohudhuria" ambao wametenganishwa. ni SASA "wamama, ndugu, dada mia



moja"—kila siku wakiunganishwa katika uhusiano wa ndani wa wapenda Nuru "kuanzia mdogo hadi mkubwa".

Hii ndiyo Habari Njema ya Ufalme wa Yesu. Alisema, "Baba Yangu anabidii ya nyumba inayojengwa." Baba anataka sana tujenge Nyumba Yake kwa njia Yake. Katika nchi nyingi na miji ni nadra sana nyumba kujengwa vile Yesu anataka ijengwe. Karibu katika kila "kanisa" karibu katika kila nchi, kuna watu wanaokuja pamoja na mila na tamaduni na kisha kwenda kivyao wakiishi maisha yao vile watakavyo. Pengine wanatenda dhambi, au pengine wanajaribu wasifanye dhambi. Lakini sio nyumba kwa sababu hao sio Familia, kila siku, kwa pamoja.

Ni wakati tu mawe yote yanapowekwa pamoja, na gundi la upendo wa kweli na uwezekano wa kudhuriwa, na kujengwa na mbuni ya Mungu, ndio inaweza kuwa mahali ambapo anaweza kupaita nyumbani. Hata kama wewe ni jiwe zuri lililohai na unajaribu kuishi maisha matakatifu, bado wewe ni jiwe moja. Nikiweka jiwe hilo mchangani, bado halitakuwa nyumba ya Yesu. Hataki mawe mazuri ya kibinafsi yakae uwanjani. Tunastahili kufanya sisi wenyewe, hata kama nikujilazimisha, tukae pamoja na mawe mengine. Kila siku lazima tujiamrishe kwamba tukae pamoja na mawe yale mengine, kila siku kwa mbinu ya Mungu ya Nyumba… tunapokuwa "tukiinuka, tunapokaa chini, tunapotembea barabani" kwa pamoja. Kuosha nguo kwa pamoja, na kwenda sokoni pamoja. Tunapofanya kazi mashambani, kutengeneza matofali, kukata mbao za kuni, au kutengeneza chakula, tufanye hivyo *kwa pamoja* ili tuwe Familia moja badala ya watu wengi au familia nyingi. Ni katika maswala haya "yasiyo na maana" ya maisha ya kila siku ambayo tunashikanisha Imani, Tumaini, na Upendo pamoja. Kazi hizi za kila siku, tukiishi kwa pamoja kama Familia, ndio "madirisha ya nafsi" ambayo huturuhusu sisi kujiosha na maji ya Ulimwengu, badala ya dini ambayo hufanya-iaminike ya "kuhudhuria" karamu za kidini na kuimba—pamoja na hotuba za mtu mtakatifu. Yesu hajengi chochote bali familia.

Yesu alisema, kwa kweli ukitii mapenzi Yangu, utakuwa na baba, mama, ndugu, dada mia moja—sio jirani mia moja, bali

washirika mia moja wa karibu sana wa familia. Hii ni mapenzi ya Mungu. Haya ni mafunzo ya Yesu Kristo—kwamba ajenge nyumba Yake na nyenzo nzuri. Nyenzo mbaya hazikaribishwi ikiwa hazitabadilika wakati zinaposikia maneno ya Yesu.

## Kujenga Ili Iwe Imara

### *Ujasiri Wa Kubadilika*

Baada ya miaka kumi ya kuwa Mkristo, watu wengi katika dini ambayo inasimamiwa na watu wa kidini, ambayo ni ya kuhudhuriwa hawana nguvu sana zaidi ya vile walivyokuwa baada ya mwaka wao wa kwanza. Hii sio vizuri. Ikiwa mtoto wetu wa mwaka mmoja akifikisha umri wa miaka kumi lakini bado hana nguvu au kuwa na hekima zaidi ya wakati alikuwa na umri wa mwaka mmoja, hiyo inaweza kuwa ya kuhuzunisha sana. Ikiwa ungekuwa na mtoto wa miaka kumi katika familia yako ambaye bado hana nguvu kama mtoto wa mwaka mmoja, na bado hawezi kutembea au kuzungumza vizuri zaidi ya mtoto wa mwaka mmoja—kama baba au mama hiyo inaweza kuvunja moyo wangu, sivyo?

Je! unadhani Baba aliye mbinguni anahisi aje wakati watu Wake Wote wanapaswa kuwa na nguvu na hekima na "wamejawa na Roho Mtakatifu na wamejawa na hekima," na "wanapaswa kuwa walimu kwa sasa" "si watoto tena," tukifanya kazi ya Mungu… ijapokuwa wengi wetu bado hatuna nguvu zaidi ya watoto wa mwaka mmoja? Hii ni kweli ulimwenguni kote, na huvunja moyo wa Mungu. Hatuwezi kuimba nyimbo za kutosha au "kuhubiri" mahubiri ya kutosha ili kubadilisha hiyo, kwa sababu hatujakuwa tukijenga njia ya Mungu katika Nyumba ya Mungu.

Mungu amembuni Nyumba Yake ijengwe ili dhambi ziweze kukombolewa na kuangamizwa. Njia ya Mungu ya "kuwa na kanisa" huruhusu uhusiano kuponywa na dhambi na udhaifu kuondolewa. Huu ni moyo wa Mungu kwa watu Wake ulimwenguni kote. Tunataka kukuambia vile watu wazuri wanaweza kufikia uwezo wao *sasa.* Tunaweza kuruhusu vipawa katika Mwili wa Kristo kujengwa pamoja katika makao ya Mungu, iliyojawa na utukufu wa Mungu. Kuna njia ambayo Mungu anataka sisi tujengwe ili tuweze kuona nguvu za dhambi zikivunjwa katika maisha ya kweli na tusiwe watumwa wa udhaifu wote wetu. Mpango wa Mungu ni kujenga mahusiano, sio kuwa na shida wakati wote. Mungu ana njia nzuri ya kujenga Nyumba Yake na watu wazuri. Hadi sasa, dini duniani kwa kawaida imejenga Nyumba ya Mungu vibaya, wanadamu wakiwa wakubwa na wanadamu watakatifu, na "kuhudhuria" mikutano kama ufafanuzi wao wa "kanisa." Tunapaswa kujua kujenga, lakini sasa lazima tujifunze kujenga. Mungu alisema "tunapaswa kuwa waangalifu sana tunavyojenga." Kuna kweli muhimu ambazo zimekuwa katika Biblia yako ambazo zitabadilisha maisha yako na kubadilisha vile kanisa linavyoonyeshwa, ndiposa kumuinua zaidi Mfalme wetu Yesu na kuona Ndoto Yake Ikikamilika!

Mungu anataka kujenga Nyumba Yake ili sisi wote tuwe wenye nguvu kwa pamoja. Anataka kujenga Nyumba Yake ili milango ya kuzimu isiweze kuishinda tena. Anataka kujenga Nyumba Yake ili mahusiano yaponywe. Anataka kujenga Nyumba Yake ili tuwe huru kuponya miili yetu, akili zetu, na nafsi zetu. Anataka kujenga Nyumba Yake ili tuwe na nguvu na hekima, na Habari Njema ya Yesu iweze kuendelea, kwa nguvu zaidi ya hapo zamani.

Je! una ujasiri wa kusikiliza mambo haya? Je! utatii Neno la Mungu unapokuwa ukisikiliza mambo haya? Je! utabadilisha maisha yako bila ya kujali gharama? Ikiwa una ujasiri wa kutii na kuhatarisha, basi endelea kusoma.



# Yesu:
## *Kiongozi na Kichwa*

### Uongozi Wa Yesu
*Katika Watu Wake Wote*

Wakristo wa uongo kwa miaka mingi wamewasukuma watu chini. Imewachukua watu wachache na kuwasukuma juu hivyo basi kuwafanya "viongozi" wengine matajiri na wenye kujulikana sana na wenye nguvu, i hali wana wasukuma watu wengi chini. Marekani, India, uholanzi, Romania, Brazili, na ulimwenguni kote, kuna Wakristo "mashujaa" na Wakristo wa "chini." Hii ni vibaya sana. Yesu aliwaambia watume kumi na wawili katika Mathayo 23 "Usimwite mtu ye yote mwalimu, usimwite mtu yeyote baba, usimwite mtu yeyote kiongozi, usimwite mtu yeyote bwana, usimwite mtu yeyoye 'rabi', usimwite mtu yeyote 'mchungaji', usimwite mtu yeyote 'mheshimiwa'—kwa kuwa nyinyi wote ni ndugu mlio na Baba Mmoja!" Hakuna "mashujaa" katika Ukristo wa Kweli isipokuwa Yesu. Hakustahili kuwa na wakubwa rasmi ambao wanasimamia maamuzi, pesa, na watu—isipokuwa Yesu na kupitia Watu Wake pamoja na Roho Yake.

Biblia inasema katika Waefeso 4 kwamba wakati Yesu alienda Mbinguni na akatuma Roho Wake, Alichukua sehemu zake Mwenyewe na kuzigawanya kwa Mwili wa Kristo, Kanisa. Yesu

alichukua vipawa vyote alivyokuwa navyo ( na Yesu alikuwa na vipawa vingi vya kiroho, sivyo?) na akawapa watu Wake wote. Hakuchukua vipawa vyote alivyokuwa navyo na akampa "mchungaji" au "mtu mmoja wa Mungu." Maandiko yanasema Alichukua Vipawa Vyake vyote na akavipa mwili Wake wote. Biblia inasema Roho huwekwa na kupeanwa kama Kipawa, kama vile Roho apendavyo, kwa Kanisa lote. Ikiwa wewe ni Mkristo wa kweli, ikiwa kwa kweli umeacha maisha yako kwa ajili ya Yesu, basi Roho Mtakatifu hukupa *wewe* kipawa maalum sana.

Na, kipawa chako ni sehemu ya Yesu. Kuna vipawa vya aina nyingi sana vilivyoorodheshwa kwenye Biblia. Kwa mfano, Roho Mtakatifu hupeana neema kama kipawa. Kipawa cha neema ni sehemu ya Yesu ambayo aliwapatia watu wengine. Ni kipawa kisicho cha kawaida. Sisi wote tunapaswa kuwa na neema, sivyo? Lakini kuna neema isiyo ya kawaida ambayo ni kipawa cha Roho Mtakatifu. Na kwa kuwa mamlaka yote ni ya Yesu na kila kipawa ambacho kila mmoja wetu anacho ni sehemu ya Yesu, basi tunanyenyekea kwa vipawa ambavyo viko katika kila mmoja wetu kwa sababu ni Yesu alivitoa.

Kwa njia hii, uongozi uko katika watu wote wa Mungu. Biblia hutuita sisi Ufalme wa makuhani. Biblia haisemi Ufalme ulio na makuhani, bali Ufalme wa makuhani. Hakuna kikundi maalum kama vile makuhani Walawi wa Agano la Kale. Katika Agano Jipya, watu wote wa Mungu wanapaswa kuwa kuhani wa yule mwingine. Kusudi la Mungu si mtu mmoja maalum mtakatifu ambaye anaweza kuhubiri. Biblia inasema Yesu alipaa juu na akapeana Vipawa Vyake kwa watu Wake *wote.* Alifanya ***Ufalme*** wa makuhani. Aliweka sehemu Zake katika kila mtu Wake ambaye kwa kweli amebadilishwa, kijana au mzee. Hiyo ndio maana tuna hitaji vipawa vya yule mwingine. Tuna hitaji vipawa *vyote* vya Yesu! Kuna mamia ya vipawa kwa sababu VYOTE vya Yesu vilimwagwa kwa Familia Yake. Hii ndio maana Yesu alisema sisi wote ni ndugu kati ya ndugu. Hatuhitaji mtu mmoja na kipawa kimoja kikisimama mbele yetu tena. Tusiruhusu hiyo tena. Wale Wake wote waliobadilishwa na Yeye anaishi ndani yao, kwa kuishi



Maisha ya kila siku iliyotakaswa kwa pamoja na wanaonekana ni Wake (Waeb. 3:12-14)—WOTE ni Makuhani!

Hakuna mamlaka fulani maalum ambayo yako kwa "mtu mmoja wa Mungu" na wale wengine wote wanakaa na kumtazama. Kwa sababu ya vile wanadamu wamejenga kanisa kwa miaka 180o na zaidi iliyopita, tumefanya kana kwamba kuna kipawa kimoja—kipawa cha "uchungaji." (Au pengine kila mtu yeyote ameruhusiwa kuwa na "kipawa cha kutoa pesa"!) Lakini uchungaji ni kipawa kimoja tu! Tukijenga vibawa, sisi wote tunapoteza. Ikiwa mtu mmoja amesukumwa mbele ili awe "mchungaji" na kila mtu mwingine anakaa chini na kusikiliza kila wakati, basi hakuna yeyote anaushiriki na kipawa chako. Wanapata vipawa vya "uchungaji" tu. Hiyo ni kidogo sana na iharibikayo! Ikiwa tunataka kuona ukubwa wa Mungu, na ikiwa tunataka kuona maisha yetu yote yakibadilika na maisha ya watoto wetu yakibadilika, tunahiji VYOTE vya Yesu. Vipawa ambavyo kila dada na ndugu anavyo ni sehemu ya Yesu. Hata watoto wana vipawa ambavyo ni sehemu ya Yesu. Tunahitaji vipawa hivyo vyote katika maisha yetu. Sisi wote ni ndugu. Moyo wa Mungu ni kuwa nipewe kipawa ambacho unacho na nikupe kipawa ambacho ninacho. Tusitosheke tu na sehemu ya Yesu. Amina?

Je! unaona ni kwa nini tulisema ni lazima uwe na ujasiri? Mambo lazima yabadilike! Hauwezi kuendelea kuyafanya yale ulikuwa ukiyafanya. Itakubidi uamue kutumia vipawa vyako zaidi na kuwakaribisha wengine wafanye hivyo pia. Itakubidi uamue kuwa mtiifu na uwe na ujasiri. Ukiendelea kukalia kiti chako au kukaa sakafuni kila wakati na usitumie vipawa vyako zaidi ya vile ulivyokuwa ukivitumia, vipawa vyako vitaendelea kupotea. "Yule ambaye amepewa imani au kipawa lazima awe mwaminifu." Je! unakumbuka kilichomfanyikia mtu yule ambaye alizika kipawa chake? Yesu alisema, "Wewe mtumishi muovu, mvivu." Hivyo ndivyo Yesu hutuambia wakati tusipofanya kile tunachopaswa kufanya. Nikikosa kutumia kipawa changu au ukikosa kutumia kipawa chako, tunakuwa "waovu na wavivu."

Je! ikiwa wewe ni mkimbiaji wa Olimpiki na umelala kitandani na mtu akachukua kamba na akakufunga? Ijapokuwa unaweza kuwa bingwa wa riadha, ukifungwa kitandani misuli yako itapungua, na mwishowe utakufa. Uwezo wako wote utapotea kwa sababu umefungwa kwa kitanda kwa miezi au miaka. je! unaona vile tamaduni za wanadamu zimeiba na kufunga Neno la Mungu? Vile tulivyojenga kwa zaidi ya miaka 1800 katika Nyumba ya Mungu imefunga watu wengi wa Mungu kwa kitanda! Hawajaweza kuamka na kukimbia na kutimiza umilele wao kwa sababu wanadamu wamejenga vibaya, hawajafuata Neno la Mungu. Tukijenga au kuunda kanisa kwa njia ambayo inamwinua mtu mmoja au "mfanyakazi" na kumaliza vipawa vya wengine, sisi ni waalifu katika Mahakama za Mbinguni kwa sababu ya uharibifu na hasara ambayo wengi watapitia kwa sababu ya "chachu kwenye mkate" na Vipawa visivyotumiwa!

Sio kwa sababu watu ni "wabaya" ndiposa tumekuwa tukijenga vibaya. Mara kwa mara ni kwa sababu hatukujua njia ya kujenga Nyumba ya Mungu na Mbuni ya Mungu. Kwa miaka 1800, ulimwengu wa Wakristo umechanganya masuala ya Mkristo ni nani… kiongozi ni nani… vile maisha ya kila siku inapaswa kuwa… na vile mikutano inapaswa kuwa. Baba yetu anataka kurudisha vitu hivi katika maisha yako sasa. Kama vile Neno la Mungu lilikuwa limepuuzwa katika siku za Mfalme Yosia, na Kweli ilipatikana imezikwa katika kifusi cha falme na tamaduni za wanadamu, kwa hivyo leo Ukweli wa Mungu, ulipuuzwa kitambo (lakini kila mara katika Biblia) unaweza kumweka mwanadamu huru. Mungu atabadilisha maisha yako kwa kimiujiza na kubadilisha kila mmoja karibu na wewe kama matokeo yake. Hii ni kweli yenye nguvu na ya dhamani sana. Aidha kuna chache au nyingi katika mji wako au boma, "Mungu hazuiliwi kuokoa wengi au wachache" kama vile Jonathani, rafiki wa karibu wa Daudi alivyosema. "Yule aliyepewa imani lazima awe mwaminifu." Lazima tuwe na ujasiri wa kufanya jambo kuhusu Ukweli tuliopuuza au tuliokosa kutii zamani. Na Yeye Mwenyewe atakuwa Mchungaji wako, Ngome yako, na Mlinzi wako unapomwishia kwa ujasiri.



# Uongozi Wa Yesu

## *Samweli Dhidi Ya Sauli*

Katika nchi zote duniani kote, sisi wote tumefanya makosa makubwa sana kuhusu uongozi kanisani. Katika sehemu nyingi mtu ambaye amesomea Biblia katika chuo cha Biblia au shule za biblia, au mwanabiashara mzuri au mnenaji, anakuwa kiongozi au "mchungaji." Tumeona nchini India na nchi zingine, wakati mwingi, kwamba mtu aliye na baisikeli ambaye anaweza pia kusoma anachaguliwa kuwa kiongozi. Hii sio njia ya Mungu! Uongozi wa Mungu msingi wake si yule anayeweza kusoma, au yule anayejua zaidi, au yule anayeweza kuzungumza vizuri kabisa, au yule ambaye ana ujuzi bora kabisa wa biashara, au yule ana mali au elimu au anayependeza au kuvutia au baisikeli.

Wacha nikufafanulie aina ya viongozi wawili tofauti kabisa. Mmoja ni kiongozi kutoka moyoni, kutoka kwa uhusiano wa sasa na Mungu. Mwingine ni kiongozi wa cheo ambaye anaweza kuwa na jina na anaweza kuwa mkubwa "mtu mkuu," mkubwa rasmi. Yesu alisema kwamba ***haipaswi kuwa*** kiongozi kwa cheo. Viongozi wa Kanisa ni wale ambao wanatembea kwa karibu sana na Mungu KILA SIKU. Ikiwa ndugu au dada hatembei kwa karibu sana na Mungu kila siku, hawezi kuzingatiwa kuwa kiongozi. Ikiwa pengine mtu wiki iliyopita hakuwa karibu na Mungu lakini ametubu dhambi katika maisha yake na sasa anaweza kumsikiza Mungu vizuri, yeye ni kiongozi zaidi wiki hii zaidi ya wiki iliyopita. "Kuwa kiongozi" hutokana na uhusiano na Mungu na watu wa Mungu. Sio kutokana na ofisi au jina. Tuna viongozi wengi katika mji tunapoishi, lakini hatuna "maafisa." Kiongozi wiki hii anaweza kuwa si kiongozi wiki inayofuatia. Yesu alisema mamlaka yote mbinguni na duniani ni YAKE. Hii bado ni kweli. Kwa hivyo, ijapokuwa tunaweza kumsikia Yesu, ambaye ana mamlaka yote, hayo ndiyo mamlaka ambayo mwanadamu anayo—sawa tu na vile anavyoweza kumsikia Yesu. Hiyo imetosha. Alisema, "Mamlaka yote Mbinguni na duniani" ni ya Yesu. Mtu ambaye hajui au kumtii Yesu anaweza kuwa "sanamu" tu. Mtu kama huyo anaweza kutiiwa kulingana na vile dhamira inavyoruhusu, ikiwa ana "cheo," lakini yeye ni "kiongozi" tu kulingana na vile anavyojua, anavyopenda, na kutii Kichwa, Yesu.

Kwa kweli kuna mfano katika Biblia ya aina ya viongozi hawa wawili tofauti kabisa. Samweli na Sauli walikuwa viongozi wa watu wa Mungu, Israeli. Samweli alikuwa mtu wa Mungu ambaye alikuwa na ushawishi katika taifa hilo kwa sababu alimjua Mungu. Samweli alikuwa na tabia zote za Mfalme wa Israeli—lakini Samweli hakuwa mfalme! Walakini, Sauli aliitwa mfalme. Israeli ilitaka kuwa na mfalme—walitaka kuwa na mtu mmoja awe mkubwa. Walitaka mtu wa kubadilishana na Samweli, na walitaka"mfalme" kama vile mataifa yaliyowazunguka. Kwa njia hiyo moja uongozi unaweza kuonekana unafanana, lakini Samweli hakuwa na "cheo" cha mamlaka. Samweli alifanya kazi kutokana na uhusiano wake na Mungu, na Sauli akafanya kazi kutokana na cheo/ofisi yake. Samweli hakuwa na ofisi, katibu, au mshahara. Hakuwa katika "cheo cha mfanyakazi" kama mfalme. Samweli alikuwa mtu wa Mungu ambaye aliheshimiwa kama mfalme, lakini hakuwa na ofisi wala cheo. Hakuwa mfalme. Hakuwa "mchungaji." Alimpenda Mungu kwa moyo wake wote. Na kwa sababu angeweza kumsikia Mungu, alikuwa na ushawishi. *Hakuwa na cheo…alikuwa na ushawishi.* Ikiwa mtu kwa kweli anamjua Mungu, atawasaidia watu wa Mungu. Ikiwa ameitwa na Mungu, atakuwa akiwasaidia watu. Nitaisema tena: Mtu wa kweli wa Mungu hana cheo… ana ushawishi. Ayubu, 29, ni ufafanuzi wa mtu aliyeheshimiwa na Mungu na wanadamu, na aliogopwa na kuchukiwa na shetani. Mtu kama huyo haitaji afisi au jina au mshahara. Ikiwa wewe ni kama Yesu, hauhitaji "nguvu" zozote.

Kwa mfano, ikiwa mimi ni seremala, ninatengeneza vitu kwa mbao. Ninatengeneza kiti, meza, au mlango kutoka kwa mbao ikiwa mimi ni seremala. Ikiwa mimi ni mwashi, basi ninatengeneza vitu kwa matofali. Kitu nilichokiunda kutoka kwa matofali ndiyo dhibitisho la kuwa mimi ni mwashi. Kitu nilichokiunda kutoka kwa mbao ndicho dhibitisho la kuwa mimi ni seremala. Hivyo pia, katika Biblia neno "mchungaji" (kwa kweli, tafsiri mbaya) hurejelea kipawa cha *mchungaji,* kinachotumika kila siku kati ya watu wa Mungu pamoja na vipawa vingine—sio ukubwa au "kichwa kinachozungumza" wakati wa mkutano. Je! dhibitisho liko wapi la kuwa mimi ni mchungaji? Dhibitisho ni kuwa nina wapenda watu wa Mungu! Nina wasaidia mchana na usiku. Si



hitaji ofisi kufanya hivyo. Si hitaji jina. Si hitajiki kuwa mkubwa. Nina wapenda watu kwa kipawa ninacho, na nina wasaidia. Dhibitisho la kuwa mimi ni seremala ni kiti nilicho kiunda. Dhibitisho la kuwa mimi ni mchungaji ni kuwa nina walisha watu wa Mungu kila siku, na wako karibu na Yesu kwa sababu yangu. Nikiona mmoja wa watu wa Mungu ana njaa, inavunja moyo wangu. Nikiona kwamba mmoja wa watu wa Mungu yuko taabani au hatarini, moyo wa mchungaji ndani yangu huwakimbilia ili kuwalinda. Hilo ndilo dhibitisho la kuwa mimi ni mpakwa mafuta wa Mungu ili niwe mchungaji. Sihitaji tepe ya jina. Sihitaji cheti kwenye ukuta na diploma kutoka kwa chuo cha Biblia. Nina hitaji moyo wa kupenda na kufanya kazi ya Mungu, na kwa hivyo nita zaa matunda ya kitofauti katika eneo lolote ambalo amenipatia kipawa.

Kwa hivyo, wewe ni seremala? Hivyo basi tengeza viti. Una kipawa cha uchungaji? Basi wapende watu—kwa kuwalisha, kuwalinda, na kuwasaidia. Hii ni kweli kwa kipawa *chochote!* Dhibitisho la kipawa chochote ni katika tunda linalo zaa.

Kwa hakika, kinyume cha haya yote pia ni kweli. Ni ukweli wa ajabu kwamba wapagani katika fani ya sayansi na madawa kwa kweli hudai kwamba wale walio na maoni na ufafanuzi na wanaojidai "wataalam" wana kitu cha kuonyeshana, tunda fulani katika maisha yao, la kuonyeshana kwamba wana haki ya kuwa papa au kufunza au kuwashutumu wengine. Katika ulimwengu wa kidini, la kushangaza, kuna uadilifu mdogo zaidi ya vile wapagani wanavyoonyesha. Walakini, katika dini, watu mara kwa mara ni vipofu zaidi na wanapendelewa. Ukosoaji, utaalam, hukumu, na hata pia uhujumu wa uhusiano na uzushi humiminika virahisi kutoka kwa wale walio na tunda bovu katika maisha yao, familia zao, na mikusanyiko yao. Ya kushangaza zaidi, lakini kweli, ukitazama dini ya mtu kwa makini na kwa uaminifu. Mtu anayefanya vitu kama hivyo kama vile kudanganya au uzushi au anayefanya kama mtaalam wa uhandisi au madawa, au biashara kwa kweli anaweza kufungwa. Lakini, katika dini wanaweza kwa urahisi kukusanya umati kati ya waogopao au wasiojua au wale ambao wanaweza kushurutishwa, kusalitiwa,

au kusifiwa ili wakubali mashine isiyozaa matunda na "wataalam." Ya kushangaza, lakini ni kweli. Hufanyika kila wakati, kwa sababu hivyo ndivyo ufalme wenye makosa uhifadhi watu wake. Uoga na sifa, masengenyo, chongezi, uzushi, au usaliti wa kihisia. Haishangazi kwamba Yesu hakufanya vyema katika dini za siku Zake zilizokuwa duniani. Lakini, tunaweza kujifunza kutoka Kwake na kukumbatia Andiko, na kutafuta Tunda, wala si sikia-sema na ajenda na mifupa iliyofichwa, bajeti, na kiburi cha kulinda.

Kwa kweli, sasa unapata wazo hilo. :)

## Uongozi Wa Yesu
### *Katika Mikutano*

Jambo lingine ambalo lazima tuwe na ujasiri wa kulibadilisha ni kuwa na mikutano kama vile Biblia hufafanua katika 1 Wakorintho 14: "Ndungu, mnapokusanyika, na Kanisa lote liko pamoja, na kila kitu lifanywe kwa kujenga Mwili. Kila mmoja wenu ana neno la kuongoza, wimbo, ufunuo." Tunapoishi kwa njia hiyo, hata asiyeamini huanguka kifudifudi na kulia, "Mungu yu kati yenu!"


Hakuna mkubwa isipokuwa Yesu! "Usimwite mtu ye yote kiongozi, bwana, mwalimu, au mchungaji. Nyinyi wote ni ndugu." Nyinyi wote mna Yesu na Yeye ni sawa kwa kila moja wetu. Kwa hakika kutakuwa na utofauti wa kukomaa, na vipawa vingine ni vya "hadharani," wakati vingine vimetulia au havionekani katika mipangilio ya umma. Lakini, vyote vinapatikana na vina nafasi. Wakati mwingine tunahitaji neema ya Yesu na wakati mwingine tunahitaji mafunzo ya Yesu. Wakati mwingine tunahitaji nyimbo za Yesu na wakati mwingine tunahitaji usaidizi wa Yesu ili kutatua shida. Lakini zote ni sawa kwa Yesu. Tafadhali soma 1 Wakorintho 14:26-40. Hakuna mwingine aliye kwenye husukani isipokuwa Yesu Mwenyewe. tunakusanyika pam0ja "tukizingatia vile tunavyoweza kuchocheana kuwadia upendo na kazi nzuri" (Waeb. 10:24-26). Lazima tuwaze na tuombe kuhusu vile tunavyoweza kusaidiana wakati tunapokusanyika, na kila mmoja



wetu achukue jukumu la kuweka Neno la Mungu na Upendo wa Mungu. Hakuna "mtu maalum" anayetarajiwa "moja kwa moja" kufanya lolote—isipokuwa kusikiliza na kumwitikia Mungu kama mtu mwingine yeyote. Mtu akileta mafunzo kutoka kwa Yesu na wengine waje na neno la uongozi au wimbo au ufunuo; ikiwa ndugu au dada anashiriki jambo ambalo Yesu alimwonyesha na ufunuo humjia mtu wa pili, wa kwanza "atakaa chini"—ikiwa tunaitikia amri ya Mungu, badala ya tamaduni za wanadamu. Daima Biblia imesema, "Wakati ufunuo unapomjia mtu wa pili, NA MTU WA KWANZA AKAE CHINI!" Hivyo ndivyo inavyosema katika 1Wakorintho 14. Hii haijulikani na wale ambao "wanapenda kuwa kwanza" na wanapenda kuwa kwenye usukani na wanao onekana kama "wa kiroho sana" na kuchukua pesa za watakatifu. Tumerithi mzigo mkubwa wa tamaduni kutoka kwa wakatoliki wa kirumi na kutoka kwa "waprotestanti" wetu na "madhehebu" na baba wapagani wa zamani. "Kuhani" au "mchungaji" au Mratibu au Afisa Mtendaji Mkuu yuko wazi, kuzungumza na mlei "wa chini"—watu wote masikini, umati wote—wakikaa chini na kusikiliza. Hii ndiyo tabia na "mafunzo" ambayo Yesu alisema anachukia—ile ya "Wanikolaitani" (ilivyotafsiriwa kama wale ambao "wanashinda Watu Wake"). Lakini MUNGU alisema hayo yote lazima yabadilike, kwa sababu Yake na yetu.

Kutoka kwa maoni ya kweli, ninataka kutoa maoni kwako kwamba ikiwa kwa kweli tunataka kuheshimu vipawa kati yetu, na kutoa vipawa ambavyo viko katika Watu wote wa Mungu, basi tunahitaji kubadilisha vitu vingi. Inaonekana ya upuzi, lakini mojawapo ya vitu hivyo ni vile tunavyokaa wakati tunapokusanyika pamoja. Wakati Yesu alikuwa hapa, alikuwa na watu karibu na Yeye. "Kwa wale waliokaa katika mviringo karibu na Yeye—hawa ndio mama zangu, ndugu zangu, dada zangu" (Mathayo 23 na kadhalika). Waliokaa kwa mviringo karibu na Yeye! Si hilo ndilo jambo la kawaida la kufanya, wakati tunapokusanyika kumsikiliza YEYE, na wala sio mtu wa kawaida aliye na vipawa vilivyodhibitiwa? Hii inaweza kuonekana kama rahisi kwako, na inaweza kuonekana kwamba si muhimu sana, lakini nina kuhakikishia ni muhimu. Nimesikia kwamba maneno ya "madhabahu" na "mnofu" yanatamkwa sawa katika Kifaransa.

Tunapokaa kila mtu akiangalia mbele, tunamzingatia mtu mmoja. Hatuko sawa kati ya walio sawa tena. Ninamfuata yeyote ambaye amechukua kiti mbele yangu kama bwana yangu, au kondakta au msaidizi au askari wa trafiki au mtaalam wa "klasi" au huduma." Tunapoweka viti kwa mistari badala ya kukaaa kwa mviringo karibu na Yesu, ni kama kumwangazia mtu mmoja. Kila mtu ni umati na mtu mmoja wa kawaida ndiye kivutio. Hiyo ni vibaya sana kwa sababu kuna vipawa vingi kati yetu, na vyote ni sehemu ya Yesu. Tukimweka kila mtu akiangalia mbele, tunainua kipawa kimoja tu. Mtu anaweza kuwa na kiburi sana kujiruhusu mwenyewe kuwa na "kiti kikuu" au kuangaziwa.





Katika mfano huu ulionyeshwa hapo chini, sawa na mifano ya dini katika taasisi na "makanisa ya nyumbani," kuna mtu wa kawaida ambaye yuko "kwenye husukani" kirasmi ambaye kila kitu lazima kipitie kwake. Yeye ndiye huanza kirasmi, anayemalizia kirasmi, anayefunza kirasmi au "anayepeana" mafunzo au "ibada." Yeye ndiye hufanya maamuzi, anayejibu maswali, na kusimamia "kazi." Hii si kibiblia (1Wak. 14:26) na haileti Matunda. Chachu kwenye mkate, Vipawa vilivyomalizwa, na Uongozi uliopotezwa wa Yesu ni dhibitisho katika mfano huu. Pia, "mbinu" kama hiyo haipatikani kwenye Biblia. Hiyo inapasa kuhukumu.



Mfumo wa ulimwengu wa tabaka (dini ***zote*** za "ulimwengu", pamoja na "ukristo wa kitamaduni") ya walai/ watu wa kanisa na "maonyesho" yaliyopangwa mapema ya kuingiliana hayapo kwenye Biblia, wala katika Roho na Akili ya Mungu. Yesu alizungumza waziwazi na kwa uzito, na hata kwa kuita majina, dhidi ya mfumo uliojawa na tamaduni na mamluki na wale wanaojiinua wenyewe juu ya Watu wa Mungu. Hata "Watume Kumi na wawili wa Kondoo" walikuwa wawe "ndugu kati ya ndugu" "kati" ya Watakatifu, sio "juu" yao, kulingana na Yesu Mwenyewe. Mungu anatamani uongozi wa Samweli, kati ya Maisha, bila jina au cheo, bali upendo na kipawa, kama inavyohitajika. Vinginevyo, "tunamkataa Mungu" kwa kuruhusu na kutamani mfano wa "uongozi' wa aina ya Sauli, kulingana na azimio la Mungu kwa Samweli, na kwa Watu Wake. Kwa hakika, huu ni mwito mkali ukilinganishwa na tamaduni za wanadamu ambazo wengi wao wamechafuliwa nazo katika maisha yao yote. Lakini, hadi tutathmini tena njia zetu na Maandiko, tunaweza tu kuendelea kuwa fugufugu sana, kuwa na matokeo yaliyojawa na chachu, kama vile dini za siku hizi hufanya.

Hapa kuna asili ya swala moja ambalo lazima tulizingatie: je! wakati wetu pamoja ni "kuhusu" Yesu au "KUTOKA" kwa Yesu? Utiifu na uvumilivu na uhuru wa Watakatifu WOTE huleta utofauti wote! *"Kwa kuwa VITU VYOTE vyatoka kwake, viko kwa uwezo wake, tena vinarejea kwake Kutoka Kwake!"* Mfano wa ukristo ulioundwa na mwanadamu wa "kuhuthuria" na "mtu mtakatifu" hudhibitisha hasara KUBWA. Yesu hapati njia YAKE ndani yako, au kupitia wewe, au kwako kama apendavyo wakati wanadamu wanapo simamia—na michezo yao ya "ubunifu" na nguvu. Njia ya kuogofya, au ya kujitangaza mwenyewe, ina faida za kifedha na huinua kiburi kwa tabaka ya watu wa kanisa. Ndio maana kuna nguvu nyingi na kuitwa majina wakati vitu hivi vinavyoletwa kwa wengi wao. Ni "Jiwe ambalo WAJENZI walilikataa ambalo limekuwa Jiwe Kuu la pembeni." "Wajenzi" ndio wale ambao wana kitu cha kupoteza. Au WANADHANIA wana kitu cha kupoteza, kwa sababu hawamwamini vya kutosha Yesu au Watu Wake. Walakini, ni hakika kabisa kwamba Yesu anazuia (Mat.23, n.k) miundo kama hiyo iliyoundwa na mwanadamu na majina yote ya

kidini ambayo inajulikana sana siku hizi. Ni aibu na hasara kubwa kwa sababu Vipawa Vyake havitumiki, na Sauti Yake haisikiki. Na hii ni kweli hata kama "mahubiri" yalikuwa "mazuri" au ya Kibiblia, au "muziki" ulikuwa wa "Kuhimiza." Nitakuepusha na "takwimu" za "tunda" mbovu linalohusiana na ukristo wa sasa, haijalishi "mahubiri mazuri" na "nyimbo za kuhimiza." Dini linalo tegemea mahudhurio, linalo simamiwa na watu wa kanisa *halijatoka* Kwake, hata kama ni "kwa" ajili Yake. Hufanya utofauti wote wa kama "milango ya Kuzimu itashinda" au kama hao WANASHINDWA na maisha Yake ya kila siku (1Wak. 12, Matendo ya mitume 2:42-47, Waeb. 3:12-14). Anataka kuwa KICHWA cha Kanisa Lake, wala sio suala la wale wanaokusanyika kwa Jina Lake.




Kwa hivyo, na je! ikiwa vipawa vyote vina sehemu sawa? Pengine kuna mtu anakipawa cha uchungaji aliyeketi kwenye mviringo. Pengine mtu aliye na kipawa cha mwalimu ameketi hapa na kipawa cha neema ameketi hapo. Kipawa cha usaidizi kinaweza kukaa hapa na mwingine aliye na kipawa cha unabii anaweza kukaa hapa. Vipawa vyote vina sehemu sawa kwa sababu vyote ni vya Yesu!



Kama tulivyojadili tayari, Paulo katika 1Wak. 14 anafafanua waziwazi wakati ambao "kanisa lote" liko pamoja. Anafafanua kuhusika kwa Watakatifu wote ambao Yesu anaishi ndani yao. Wakristo, kama ilivyofafanuliwa dakika chache zilizopita katika barua hiyo (mlango wa 12), ambao wanaishi kila siku kwa pamoja chini ya Uongozi Wake ***wanapaswa kuendelea kuishi kama Makuhani*** wakati kanisa liko pamoja katika mahali pamoja. Wote wana nafasi ya kumwitikia Yesu na Uongozi Wake wa sasa, kama Makuhani wa kweli, wakati wowote kanisa liko pamoja. Hakuna uonevu au wanaume au wanawake wa kidini walio chaguliwa mapema wakitoa hotuba iliyopangwa mapema au onyesho la wimbo. Mfano huu wa "wakati ufunuo unapomjia wa pili, na wa kwanza AKAE CHINI" ni kulingana na Picha ya PEKEE katika Agano Jipya la Uongozi wa Yesu katika Mikutano katika "Ufalme Wake wa Makuhani." Vipawa vyote vilivyomiminwa juu ya Mwili wa Kristo, Kanisa, vinaweza KUTUMIKA wakati WOWOTE. "Wakati ufunuo unapomjia wa pili, na wa kwanza AKAE CHINI!" asema Bwana. Hakuna nafasi ya kusimamia mtu au kile kinachoweza kutendeka, kilicho pangwa mapema kwa ajili ya kukaririwa au muziki, au burudani, au sababu za kudhibiti.

Katika Kanisa ambalo Yesu anaonekana kwamba yuko sasa, anahusika, na yuko Hai, badala ya masalio ya kihistoria kupendwa na kuheshimiwa na kufunzwa kuihusu, kuna Uhuru. Kila mtu ambaye Yesu anaishi ndani yake na anayetumika hivyo *kila siku* kati ya Waumini, ana jukumu la kutoa Vipawa vyao "ili kuadilisha Mwili." VYOTE vya Yesu vilimiminwa juu ya Mwili Wake, kwa Vipawa Vyake VYOTE—na Kipawa chochote kinaweza kuhitajika wakati wowote. Kijana mdogo akiwa wazi kuhusu ugumu katika mahali pa kazi, au dada akikubali kwamba ana ugumu na watoto, Vipawa vya Ualimu, au Himizo, au Uchungaji, au Usaidizi vina weza vyote kutokea, wakati "Ufunuo unapomjia wa pili!" Hii ndiyo "Picha" ya pekee ya wakati "kanisa lote liko pamoja" kwenye Biblia. Na katika "picha" hii Yesu ameruhusiwa awe Kichwa KILICHO HAI cha kanisa Lake mwenyewe, badala ya shirika lililoundwa na mwanadamu, linalosimamiwa na wanadamu wa kawaida.







Kila mtu ambaye Kristo Aliyehai anaishi ndani yake lazima awe Huru kuguswa na kutumiwa na Yesu katika kuitikia kile kinachofanyika sasa. HIYO peke yake ndiyo "Mwili wa Kristo." Basi "Mikutano" lazima iwe mfuriko wa yale yanayofanyika kwa sasa kila siku katika Maisha ya Umoja wa kila siku wa "nyumba kwa nyumba" katika Yesu. Lazima kuwe na sehemu ya YESU ya kutawala na kuongoza WATU Wake na Vipawa Vyake KILA WAKATI, katika nyumba na "mikutano." Wanadamu watajaribu kuiga kwa kutoa zawadi ya "muda wa huduma"—chochote kile—lakini hao wanabaki wakiongoza. Usikubali ujanja wowote wakati YESU anaweza kuishi kupitia Vipawa Vyake vyote na Watu.

Roho YAKE ya "Ufalme wa Makuhani"—na Yesu kwa kweli kama Kichwa cha Mwili Wake—ndiyo suala letu hapa. Na, kwa hakika, mjadala huu si kuhusu toleo fulani la kitoto na lisilo



la Kibiblia la "wakati wa wanaoanza" na kila mtu "kuchukua wakati wake" na "kushiriki kutokujua" na maoni, au "kila mtu anapaswa kusema kitu" na "ikiwa ulizungumza zaidi ya dakika 5 'wiki iliyopita' basi huwezi kuzungumza 'wiki hii', blah blah. Bila shaka Kanisa Lake si la "kidemokrasia." Kanisa Lake linapaswa kuwa la makasisi ambapo KUPAKWA MAFUTA na VIPAWA na MAWAZO YAKE YA SASA Yanatawala maingiliano yetu katika njia za kushangaza na zinazobadilika kila wakati ambazo hazina mpango. Wakati mwingine (bila mpango) mtu mmoja anaweza kumwitikia Mungu kwa sauti kubwa kwa kipindi kikubwa cha wakati. Lakini kwa sasa au tena "hatarajiwi".

Kuna uhuru na kutii Njia Zake katika 1Wak.14. Lakini, zingatia kwamba Paulo pia alizungumzia katika mlango huu dhuluma ya watu wakipuuza uongozi, au wakichukua nafasi ya "uhuru" wao kwa ajili ya tamaa au hisia au ukosefu wa hekima. Tena, kumbuka kwamba muktadha wote wa 1Wak. 14 unajumuisha "milango" 10-13, ambapo Moyo wa Mungu ni wa kuwa Watu Wake waishi kama "mkate mmoja" wakipambanua Mwili na kuishi maisha yao KILA SIKU wakiunganishwa kama vile mkono umeunganishwa na vidole na kilimbilimbi. Katika muktadha huu wa *MAISHA* ya Biblia kanisani,1Wak. 14 inaweza pia kutiiwa. "Wakati ufunuo unapomjia wa pili, na wa kwanza AKAE CHINI!." Hakuna "onyesho" na hakuna "mtu mtakatifu" aendeshae onyesho. "Yeye ni yule jana, leo, na hata milele!" Uoga, ulafi, nguvu, na tamaa ya wachache haiwezi kuruhusiwa iwaibie Watu Wake Urithi wao. Yesu yuko HAI na ANAZUNGUMZA kupitia Vipawa Vyake "kama Apendavyo" wakati sisi kwa kweli ni Mwili Wake, badala ya kufanya karamu siku takatifu.

Ndio, wanaweza kuwa "wakuu" wanaohudumia na kusaidia kuwezesha. Na, ndio, kutakuwa na wakati wa "matangazo" kwa wasio amini hadharani kama Paulo alivyofanya katika hali zingine zilizorekodiwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Bado, tofauti na siku hizi, hata wakati wa "matangazo" kulikuwa na "mazungumzo" (Neno la Kigiriki la kile kilichofanyika katika Troasi)—wala sio "mazungumzo binafsi" ambayo hauwezi kuingilia. Na aina hii ya hali ya "matangazo" na wasio amini katika

Efeso au Atheni haipaswi kuchanganywa na wakati ambao "kanisa lote liko pamoja." (Ijapokuwa, kwa hakika, wasioamini mara kwa mara watakuwepo wakati Familia ya Mungu iko pamoja (1 Wak. 14.) Wakati ambao Mwili wa Kristo unafurahia kwa pamoja katika mahali pamoja ni tofauti kabisa na wakati mtu "anahubiri mtaani" kwa umati wa wasioamini walio kusanyika. Kama mfano mmoja, Paulo alitumia "shule" ya wapagani kwa madhumuni ya kuzungumza na wasioamini kuhusu Yesu ( Matendo ya mitume 19:8-10), akieneza Neno la Mungu "kwa kila mtu katika Mkoa wa Asia." Hakika hii, ni tofauti na wakati kanisa, la walio kombolewa na Anaoishi ndani yao, wanakutana pamoja kama katika 1Wak. 12-14 au Matendo ya mitume 20 ambapo Paulo "alizungumza binafsi" (kama vile neno la Kigiriki lilivyotaja) na Familia yake hadi asubuhi katika mazingira yasio rasmi.

Yesu anatamani kujenga Kanisa Lake hadi milango ya Kuzimu isiweze kuishinda! "HIVI NDIVYO watu wote watajua nyinyi ni Wafuasi WANGU." Anataka sisi WOTE kwa pamoja "kuwa makao" Yake—kila siku, kwa kujumuishwa "na kuunganishwa pamoja" na "kushindania Imani kama Mtu Mmoja." Na katika uhusiano huu wa ndani wa *kila siku* wa "mama, ndugu, dada" Uzuri wa Maisha ambayo Yesu alianzisha, BASI Watu Wake wote (kutoka kwa mfuriko wa maisha yaliyounganishwa kabisa ya "kila siku", Matendo ya mitume 2:42-47, 1 Wak. 12-13) INAWEZA kutumiwa na Roho wa Kristo, wakati wowote. Kwa kweli ni rahisi. :) Ni kama vile alivyokuwa hapa na sisi kimwili, YESU ndiye aliyezungumza. Wakati hatumalizi Roho Wake na mipango iliyoundwa na mwanadamu na mfumo wa tabaka na ibada na tamaduni na ujuzi, na maisha ya kibinafsi ya kidunia, Yeye yuko huru kujionyesha Mwenyewe na Vipawa Vyake, kama vile alivyokuwa hapa kimwili. Mawazo na Upako Wake wa sasa, kwa muda au "hadi asubuhi"—ndiyo tamaa yetu. "Wakati Ufunuo unapomjia wa pili, na wa kwanza akae chini….!"



# Uongozi Wa Yesu
## *Kimaisha*

Baada ya kusema hayo yote, ni muhimu kusema tena kwamba haya yote si muhimu ikiwa hakuna Ubora wa Maisha ya kila siku kama ilivyo fafanuliwa katika Wak. wa kwanza 12-13 kama hitaji la "mlango wa 14." Kwa kweli, bila Maisha hayo ya kila siku hii ni "hatari." Hatuwezi tu kuzungumza kuhusu "mikutano" bila kukosa kitu muhimu sana. Suala ni kubwa zaidi. Hii ni kuhusu Ukubwa wa Maisha ya Yesu kwa Watu Wake! Na maisha ya kidunia, ya kutenganishwa, ya kibinafsi ya watu wa kidini ndio kwanini onyesho lilopangwa mapema na mtu mtakatifu linakuwa "ulinzi" wa kawaida wa wanadamu wenye dhambi ambao ni wageni, walio na macho ya mwitu wakitumia "uhuru" kama jukwaa la tamaa zao. Ubora wa maisha ya kila siku, 1 Wak. 12-13, ni hitaji na wazo la Uhuru katika1Wak. 14.

Ni lazima tuunganishe "picha" hizi za awali kuhusu wakati ambao Watakatifu wako pamoja kama Ukuhani badala ya "umati", na Maisha (Waef. 3:10) yaliyokusudiwa kila siku ya Matendo ya mitume 2:42-47, 1Wak. 12, Waeb. 3:12-14, na "mama, ndugu, na dada, MIA MOJA." Yesu alisema huu NDIO Mpango. **Ni Ubora wa Maisha ambao amewaita Watu Wake waishi kwa pamoja ndio uko hatarini hapa, "sio mpangilio wa mkutano"!** Anatamani Urithi, wala sio "mkutano" au "ubadilishanaji wa ufahamu" au kuimba kihisia". Moyo Wake ni wa Mtu Mmoja, Luka 9:23-27, 57-62—Ukristo wa kweli, "kutoka kwa mdogo hadi mkubwa" avalishwe kwa Roho YAKE.

Si kuhusu kutulia kidogo na kuwa rahisi kuwa na mikutano yetu iliyopangwa au isiyopangwa, na kuipatia lile jina la "kuongozwa na Roho." Kwa sababu hatujui mapema kile tutakaloenda kufanya haimaanishi kwamba vitu vitakuwa "vikiongozwa na Roho." Vigumu. Si KITU kama hicho. Ijapokuwa "kama vile Yane na Yambre," waongo, wakiangaliwa kutoka kwa maoni ya kidunia, inaonekana sawa na mambo ya Kweli.

Utofauti kati ya kubadilisha dini ya madhehebu, dhidi ya kuishi katika kweli ya Yesu aliye fufuka, aliyehai… inatatanisha.

Kurekebisha "mikutano" na "muundo" (katika jengo la kidini, au ndani ya "nyumba") sio muhimu vile, ikilinganishwa na Nafasi aliyotukabidhi mbele yetu hivi leo. Hatuiti kwa muundo "mpya na uliyoboreshwa." Anatuita kwa uhusiano wa kila siku wa kula pamoja kutoka kwa Mti wa Uzima, na Mpakwa mafuta! Ah, NDIO, hiyo itabadilisha "mikutano" yetu—lakini hilo ni Tunda, sio lengo. Kubadilisha kwa mafunzo, mbinu, elimu, mwendo mpya na iliyoboreshwa, vile watu wanavyoishi pamoja kwa karibu, "pochi ijulikanayo" isiyo ya Kibiblia, au idadi yoyote ya njia mpya za jadi na desturi, kwa kweli hazina maana. Kwa kweli kile tunachokifuatia (ikiwa tunatamani kile Yeye Anachokitamani!) ni Makao ambayo YESU anaweza kuishi na "kuenea" (Ufun.1-2) bila kuzuiliwa, kama MFALME anayetawala, aliyehai. Hii peke yake ndiyo MAISHA YA ZOE (kama Yesu alivyoiita). Maisha ya Kibinguni, isiyo ya KAWAIDA, isiyoweza kuangamizwa na asili ya Milele, yote ikijumuisha Ukweli wa Ufalme usio onekana wa Nguvu na Kweli na Upendo na Uzima. Yesu alileta "Uzima tele," Mito ya Maji Hai" Uzima kwa Watu Wake kutoka kwa nafasi nyingine, Ulimwengu ambao hauwezi kuonekana na macho ya mwanadamu na frikwensi ya mwanga wa kidunia.

Uzima ndani ya Kristo kwa Pamoja si kuhusu "jinsi ya kuwa na mikutano." Kile Yesu alileta Duniani na Matangazo ya Malaika haiwezi kuwa ya kijuujuu na ya nje kama hiyo yote. "Mikutano"—ambapo watu wengi wanaweza "kuhusika"—je! HIYO ndiyo Yesu alikufa kwa ajili yake? HAPANA! Yesu hakuja ulimwenguni ili kuleta njia mpya ya kuwa na mikutano au "kuwa na kanisa" au "mfumo" fulani. Hiyo haifai kabisa ikilinganishwa na ***"Malengo Yake, sasa kupitia Kanisa!"*** *(Waef. 3:10)*. Anataka kumwangamiza, kumwua, na kumwaibisha adui hadharani—na kubadilisha maisha baada ya maisha baada ya masha, kwa tabia na Maisha na Hekima na Nguvu ya Mwana. "Anawaleta wana wengi kwa Utukufu"—sio kwa Wokovu tu. Analijenga KANISA Lake, ambalo milango ya kuzimu HAITALISHINDA. Kwa Neema ya Yesu Kristo na kwa Utawala Wake, tuna warudisha wana na binti zetu na familia na majirani kutoka kwa upotofu na utumwa wa shetani. Maisha yanabadilika. Alituletea Ufalme mpya kabisa ili tuishi kando Yake—hewa mpya ya kupumua, macho mapya ya kuona, masikio mapya ya kusikia, na moyo mpya wa kuhisi na kupenda. Utofauti huu unaathiri kila kitu maishani, pamoja na "mikutano"!



Je! unaweza kuona kwamba hii inahitaji ujasiri? Je! unaweza kuona kwamba hii inahitaji imani na utiifu? Je! unaweza kuona kwamba hii itabadilisha maisha yako ikiwa utaanza kuishi katika vitu hivi? Hauta fungwa tena kitandani! Sisi ni Ufalme wa Makuhani kila siku. Na, kwa kweli mikutano ni ya ziada. Asilimia tisini ya kukua hutoka kwa kuishi pamoja, na pengine asilimia kumi hutoka kwa mikutano. Hiyo ina maanisha kwamba una stahili kutoka kwa nyumba yako na uingie nyumba za watu wengine. Unaleta maji, au chakula, au nguo nyumbani kwao. Wakati unapoona wana njaa pamoja na mtoto, una stahili kuwaweka kando na uzungumze nao na utembee nao. Unapoona kiburi katika maisha yao, wakumbatie na uwaulize wasiwe na kiburi. Unapoona uchoyo katika maisha ya ndugu, mkumbatie na useme, "Tafadhali usiwe na uchoyo tena." Hatufungi tu macho yetu hadi asubuhi inayofuatia. Tunaishi katikati ya maisha ya kila mmoja kama makuhani wanaofanya kazi ya Mungu, na kama "mama, ndugu, na dada mia moja." Hii pia, ni amri kuu kutoka kwa Mungu katika Waebrania 3, na katika maandiko mengine, mengi, mengi.

(Waebrania 3:12-14: "Angalieni, ndugu zangu. Usiwe katika mmoja wenu moyo mmbovu wa kuto kuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho."

Gundua yale Andiko hili linasema—hii ni kutoka kwa Mungu. Mungu Mkuu anakwambia wewe na mimi kwamba tunapaswa kuonyana kila siku na kusaidiana. Tunapaswa kushikamana kila siku. Roho Mtakatifu amechagua kusema "kila siku." Hakusema kila Jumapili. Hakusema kila Jumapili na Jumatano. Hakusema pia katika mikutano. Alisema muhusike katika kiwango cha kweli katika maisha ya kila mmoja. Ikiwa wengine wanapatikana au wanaweza kupatikana, na usihusike kwa sababu ya mtindo wa maisha, au kiburi, au uchoyo, au chaguo la hali ya kimaisha,

Mungu alisema utakuwa mgumu na hautaweza kuhisi Yale anayohisi. Utadaganywa kwa kudhania kwamba unajua kinachofaaa wakati haujui. Hivyo ndivyo Maandiko yanasema haswa! Hakusema tu ufanye hivyo. Alisema *ukikosa* kufanya hivi, itakuumiza pakubwa. Ikiwa sina ndugu anayezungumza na mimi kila siku kuhusu maisha yangu—*kila siku*—nitakuwa mgumu. Nitadanganyika. Lazima useme, "Lakini ninasoma Biblia yangu kila siku!" "Lakini nina omba kila siku!" "Mke wangu ni Mkristo na ninamwona kila siku!" Hivyo sivyo Mungu alivyosema. Unaweza kusoma Biblia yako na kuomba kila siku, lakini ikiwa hauta husika katika maisha ya yule mwingine kila siku, utakuwa mgumu zaidi na zaidi, na utadanganyika zaidi na zaidi. Mungu anasema haya katika Waebrania 3:12-14. Je! Unaamini Biblia? Je! Unamwamini Mungu?

Je! Ni nani aliyeiandika Biblia? Mungu! Mungu alisema kwamba tunastahili kuhusika katika maisha ya yule mwingine kila siku. Ukiniona nikiwa mchoyo, unastahili kuja kwangu na useme, "Ndugu, usiwe mchoyo. Hiyo inamuhuzunisha Yesu." Ukiniona nikiwa na kiburi, tafadhali nisaidie na unikumbushe kwamba Mungu anawakataa wenye kiburi. Sitaki Mungu anikatae! Unastahili kunisaidia, kwa sababu siwezi kuiona kila wakati. Hakuna awezaye. "Mwonyane kila siku, ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu." Hii ni sehemu muhimu (na isiyo tiiwa kabisa ulimwenguni kote) ya maisha yetu ya kila siku pamoja. Hii ndiyo njia moja kuu ya kwamba wewe ni kuhani unayetumia vipawa vyako, na "mjumbe wa Kristo, kana kwamba Mungu alikuwa akikata rufani Yake kupitia wewe."

Ukitumia kweli hizi ambazo zimekuwa daima katika Biblia yako, utashangazwa vile utakuwa karibu sana na Yesu miaka miwili ijayo kwanzia sasa. "Mwonyane kila siku." Jihusishe na watoto wa yule mwingine na ndoa na sehemu za kazi "kila siku." Enda hapo! Ni lazima utoke "mahali pako pa starehe" na uende hapo wakati ambapo haungeweza kufanya hivyo mbeleni! Ndio, nina maanisha WEWE! :) Tafadhali, kwa ajili ya Yesu! Sema Neno "kama Mungu" katika maisha ya yule mwingine, kwa kweli, kwa upendo, kwa njia ya hekima, kila siku. "Mnapo kusanyika pamoja, ndugu, *Kila mmoja* wenu ana neno la kuongoza, wimbo, ufunuo." "Wakati ufunuo unapomjia wa pili, na wa kwanza akae chini!." Unapotembea hivi, unaweza kupata kwamba wengine ambao ulidhania walikuwa Wakristo hawampendi Yesu kama vile ulivyodhania wanampenda. Unaweza pia kupata kwamba wengine ambao ulidhania walikuwa wadhaifu sana wanakuwa na nguvu na wenye hekima zaidi ya vile ungeweza kudhania. Njia za Mungu za kufichua utapeli na uongo, na kufanya wadhaifu kuwa na nguvu sana. Atukuzwe Mungu!



Utajiri huu umepewa wewe. Zitumie kwa ajili ya Yesu. Ni lazima ufafanue Mkristo kwa kweli ni nani na yale Yesu alisema. Ni lazima ufahamu uongozi na vile una stahili kuwa. Ishi maisha yako kila siku, kwa pamoja, mkihimizana, mkijengana. Saidianeni kukua na kumpenda Yesu zaidi kila wakati mchana na jioni. Kujeni na mkutane pamoja karibu na Mfalme Yesu.

Biblia ni kweli kwa asilimia 100. Ni kuhusu Yesu na Wafuasi wake. Hizi ni hadithi ya vile wanavyo umia na vile walivyo jifunza katika masaibu yao na Mungu. Kwa hakika tunaweza kujifunza kutoka kwa hadithi hizi, lakini pia tunaweza kujifunza kwa njia sawa na vile walivyo jifunza: kwa kumkabili Mungu kwa pamoja katika maisha yetu ya kila siku. Kwa ufahamu huo, hata sisi ni "waraka uliohai." Kusoma kwote duniani hakuwezi kutu badilisha sisi kama vile masaibu ya pamoja ya Maisha yanaweza kutu badilisha sisi. Mambo ya ndani tunayotaka kuyajua hayaingii kabisa ndani ya mioyo yetu wakati tusomapo kutoka kwa karatasi. Tunapotekeleza mambo kila siku, Yesu anatufunza mafunzo ya ndani ya maisha ambayo hatuwezi kusoma kutoka kwa mafunzo yote ya Biblia ya ulimwengu, ijapokuwa kweli hizi ziko katika Biblia ya kila mtu. "Nguzo na msingi wa Kweli ni eklesia—kanisa." "UZIMA unakuwa Nuru ya wanadamu."

Maisha hayakukusudiwa kuwa kama shule ya sarufi ambapo tunajifunza mawazo na kisha kuamini orodha fulani au "imani" ya mambo. Badala yake, Mungu ametuita tuwe wanaume na wanawake sawa wa Mungu kama wale waliokuja mbele yetu—tuunganishwe na Mungu Mmoja kama hao—kwa upendo na Yesu

yule mmoja kama hao. Ndiposa kufanya hivyo, hatuhitaji tu kujua yale wanayojua, lakini tunahitaji kuhisi wanacho kihisi. Ndiposa kuhisi wanach okihisi, lazima Mungu atupeleke Safari moja na yao. Kwa hivyo tunaenda safari hiyo kwa kutumia Neno la Mungu kwa pamoja katika maisha yetu. Tunaenda safari hiyo na machozi machoni mwetu, na udhaifu wetu na nguvu zetu, tukipendana, na tukisaidiana—kwa wakati mbaya na wakati mzuri—macho yetu yakiwa kwa Tumaini letu, Masihi wetu. Daimi sisi tunasonga mbele, tukimwamini Mungu kwamba atakuwa mwezesha wetu, akitusaidia tunapoishi pamoja.

Ikiwa unampenda Yesu na ujenge kwa njia sawa, milango ya kuzimu haitalishinda. Dhambi itaangamizwa. Udhaifu na magonjwa yataponywa. Dhambi zitasamehewa. Ukarimu utawaongoza wengi kwa toba. Mahusiano yatajengwa au kurudishwa, zaidi ya vile ungeweza kudhania katika ndoto zako za ajabu. Utang'aa kama nyota duniani, ukionyesha wema wa Mungu. Na Bi-arusi, Kanisa, "atajiandaa" na kuwa tayari wakati Bwana arusi atakaporudi!! Amina?

## Kusudi La Mungu … Sasa!

Nilikuwa nikitazama filamu kuhusu Albert Einstein. Ikianza kulikuwa na kifungu kilichosema kitu kama, "Kila wakati baada ya mda mrefu sana, mwanadamu huja na kuona ulimwengu kupitia macho tofauti na kubadilisha ulimwengu anamoishi." Tunataka kuweka changamoto hiyo mbele yako. Kuwa aina ya mtu yule ambaye Anaona ulimwengu, sio kupitia kwa macho ya kawaida, bali kupitia macho ya Kiroho. Pata changa moto ya kuwa mmoja wa watu wale ambao Waebrania 11 inawazungumzia kuwahusu. Ona maono ya Mungu ya makao ya Mungu na roho na utukufu unaoongezeka daima. Ona picha katika macho ya akili yako, kama inavyosema kwamba waumini katika kitabu cha Waebrania 11 walivyo ona. Waliona Mji ambao Mjenzi na Mtengenazaji alikuwa Mungu, na kwa hivyo hawakurithika na kitu kingine chochote. Hawakuwa tayari kurudi mji wa zamani. Waliona Mpango wa Mbinguni kwa mbali, na hata kama hawangeweza kuishika na mikono yao, hata kama hawangeweza kuishi ndani



ya Mji huo ambao Mungu aliwapangia, hawakuwa tayari kurudi nyuma. "Kwa hivyo, Mungu hakuona haya kuitwa Mungu wao na hao watu Wake."

Chango moto hiyo moja iko mbele yako wewe na mimi. Angalia dunia unayoishi, ulimwengu unamoishi, na haswa "kanisa" ulilo ndani yake na utamani Nyumba ya Baba ikuchukue. Na tamaa Yake ikuchukue kwa njia ambayo utakuwa tayari kuhatarisha kila kitu katika maisha yako ndiposa uone hiyo ikikamilika katika mazingira yako. Unaweza kuhatarisha maisha yako. Unaweza kuhatarisha familia yako (Zaburi 69:8-9). Unaweza kuhatarisha kazi yako. Unaweza kuhatarisha ***kila kitu*** kwa ajili ya Mungu na madhumuni Yake. Hapo ndipo tunapotoka. Kuzungumza Kibiblia hiyo kwa kweli ndiyo aina ya pekee ya Ukristo uliopo. Hilo si fikra au wazo linalojulikana sana. lakini katika Warumi 4 inasema , *"Wale waliyo na imani ya Ibrahimu ni wana wa Ibrahimu."*

Kwa hivyo, haijalishi hali yoyote ile au kanisa ulioko, na mahali unaweza kuwa ( nchi yoyote au makao ambayo unayo na uitayo nyumbani kwa sasa), unastahili kuwa mwangalifu sana ili usikubali chochote ambacho Mungu hakubali. Usikubali kwa ajili ya uvivu, kutokujua Neno la Mungu, au ukosefu wa maono au dhambi katika maisha yako ya kibinafsi ambayo imekuziba au kukujeruhi hadi unahisi hautoshi. Usiruhusu wengine ambao wametoshelezwa na Lao wakusaliti au kukukejeli ili uwe fugufugu.

Pengine umeuziwa ukweli kwamba wewe ni "walai" tu na hauna chochote cha kutoa. Pengine unadhania maoni yako hayana umuhimu kwa sababu kuna watu wengi huko nje wenye hekima na waliosoma… "Wewe unajua Ni nini?" Ninataka kukuhimiza kwamba haijalishi wewe ni nani, una kitu cha kutoa. Ikiwa kwa kweli umeitwa kwa jina la Bwana na umemwuliza achukue usukani wa maisha yako, una kitu cha kutoa. Ikiwa umemwuliza akuoshe dhambi zako, una kitu cha kutoa. Haja Yake ni kwamba kuanzia mdogo hadi mkubwa na kila mtu amjue Yeye, aishi katika baraza Lake na ashiriki na Yeye, na Utatu, kila siku.

Mara moja baada ya muda mrefu sana, mtu huja au watu huja ambao wako tayari kushuku ulimwengu wanamoishi na kufanya utofauti katika ulimwengu ulio karibu nao. Waebrania 11 inahusu hiyo. Hiyo ndiyo Mungu ameitia kila mmoja wetu awe ikiwa tuna ujasiri na tuko tayari na tunaushirika na kichwa. Tukikaa ndani Yake, kutakuwa na matunda ya kuonyeshana. Unaweza kuwa mtu ambaye analeta utofauti katika ulimwengu ulimokuwa.

Ninatumaini tumeweka wazi kuto kuelewa moja ambayo imengia katika jamii ya Wakristo. Hiyo ni kwamba kuwa Mkristo ndio mwisho wa hadithi. Na kisha "kuhudhuria kanisa unalolipendelea Jumapili" ni udumishaji hadi Yesu arudi tena na wewe uende kwa nyumba ya kifahari juu ya mlima. Ninataka kuliondoa wazo hilo kabisa kwa sababu hilo *si* wazo la Mungu. Mungu anaita wazo hilo dini la uongo na Laokia, ambalo linatatiza tumbo Lake.

*"Kusudi la Mungu ni kwamba sasa, kupitia kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulishwe viongozi na wenye mamlaka katika ufalme wa mbinguni…." Waefeso 3:10*

Hili ndilo kusudi la Mungu SASA HIVI. Mapenzi Yake ni kufanya hekima Yake iliyo ya namna nyingi ***ijulikane kupitia Kanisa.*** Sio kupitia watu ambao wameokoka, na wala sio kupitia jamii ya watu wasiyo weza kuzaa ambao wanasikiliza mahubiri siku maalum ya wiki wakiwa wamevaa suti na tai… lakini kupitia kitambaa cha maisha, kupitia jamii ya waumini ambao "wameunganishwa na kushonwa pamoja na kila kano ya kushikilia," na watu ambao vipawa vyao vimeunganishwa sana, hao "wanashirikiana." Kuunganishwa, kwa "moyo mmoja, akili moja, kukubaliana pamoja, na kusudi moja." Pigania maono hayo kwa Matendo ya waumini kutochukua mali, kwa kuunganishwa pamoja—kwa "kujitolea kwa mafunzo ya mitume, kumega mkate, kushirikiana, maombi," na "kila siku hadharani na kutoka nyumba hadi nyumba." Fikiria Watu wa Mungu kama ushirika—uliounganishwa, ulio na kitambaa cha maisha cha pamoja ambacho milango ya kuzimu haiwezi kuishinda. Dini ambalo msingi wake ni "mahudhurio" ni sawa kwa Waindi na Waislaamu, lakini sio ile Yesu aliyonzisha na kupaka mafuta.



Kusudi Lake ni "sasa, kupitia Eklesia," kupitia Ushirika ambao ni wa kweli na wala sio umati wa watu ambao wanahudhuria kitu, bali maisha ambayo yameunganishwa—"kuungamiana dhambi," kubebeana mizigo" na "kupendana." Hiyo ndio aina ya maisha ambayo wanadamu wanaweza kuona. Hayo ndiyo aina ya maisha ambayo Yesu alizungumzia kuhusu wakati aliposema "kwa upendo wetu sisi kwa sisi" kuwa "watu wote watajua" imetoka mbinguni (Yohana 13). Alisema kwamba hiyo inaweza "kuaibisha ufalme na mamlaka." Kusudi la Mungu ni sasa ***"kupitia Kanisa"*** ili kuleta aibu hadharani kwa shetani na falme na mamlaka yote. Na kusudi Lake, kulingana na maandiko, ni *"SASA"* kupitia kanisa ili kuwafanya Adui wake wawe chini ya miguu yake—sio tu kuja Kwake kwa pili na Ufalme mkuu wa Milele, kazi ya Mungu iliyokamilika, bali SASA.

Na kwa hakika, hatuzungumzii juu ya jamii kamili. Hatuzungumzii kuhusu sera za jamii, wala sio jambo la baada ya milenia, sio masomo ya utawala. Sio kunyumbua misuli, bali kando na hayo… Tunazungumza kuhusu Watu wakionyesha Maisha ya pamoja kwa njia moja na vile Yesu alionyesha maisha Yake, kama Mfalme wa wafalme wote. Alizaliwa mtoto wa haramu horini, akipanda punda aliye azimwa, na hakuwa na mali yoyote Yake—hakuwa na nguvu, hakuwa na elimu, hakuwa na jukwaa la kisiasa, hakuwa na "urembo au ukuu ambao mtu yeyote angevutiwa." Tunazungumzia kuhusu kuwa mpenda watu aliyetoka mashinani ambaye angeweza kuona mioyo ya watu na kuwaleta msalabani. Tunazungumza kuhusu kuonyesha watu kashfa ya kuwepo Kwake na maisha Yake, na kuwaita wawe wavuvi wa watu. Wawe sehemu ya Nyumba Yake, "makao" Yake. Wawe mawe yaliyohai. "Ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa." Huo ndio moyo wa Mungu.

Pokea Yesu wa Nazareti, na Ufalme "usio wa ulimwengu huu", sio kama mshinda Roma au nchi yoyote tunamoishi, au mfumo wa "kanisa." Mpokee kama Mfalme Seremala aliyependa, na kusemehe, na kutoa maisha Yake…. na yule aliyekuwa tayari kupindua meza za hekalu na kutoa fimbo kama ingehitajika kwa upendo wa Baba Yake na kwa ajili ya Nyumba ya Baba Yake.

Yesu alikuwa tayari kushuku ulimwengu alimokuwa na kwa hivyo kuibadilisha, na ametuita tuwe watu wa aina hiyo. Hii si upitishaji wa habari. Huu ni mwito wa utakatifu na utakaso wa madhumuni ya Mungu, na mwito wa kuinua maono Yake katika mioyo yenu na katika maisha yenu. Piga magoti na uombe. Huu ni mwito, si wa kubadilisha ulimwengu unao onekana tu, bali pia kubadilisha ulimwengu usionekana. "Kusudi Lake ni ***sasa*** kupitia Kanisa ili hekima Yake ijulikane, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi, kwa falme na utawala" na kwa watu wote....

*Kwa hivyo, hebu kaa linalochoma lisafishe midomo na moyo wako, mwangalie Mungu, na umlilie "Niko hapa, nitume!"*